CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

(MOCKS TRIALS 1-10)

SERIES 1 COMPILATION OF RECENT TOP CROSS-COUNTRY KISWAHILI MOCKS IDEAL FOR KCSE REVISION PURPOSES.

KCSE MODEL MOCK TRIALS

SERIES 1

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP

0707550000 / 0705525657

MWALIMU PUBLISHERS

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 1 PAPER 1

TIME: 2 ¾ HOURS

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

Karatasi ya 1

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

1. *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
2. *Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*
3. *Kila insha isipungue maneno 400*
4. *Kila insha ina alama 20*
5. ***Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.***

MASWALI

1. Jopo linaloshughulikia undanganyifu katika mithani ya Kitaifa (KCSE) limekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanajopo watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha undanganyifu, madhara ya undanganyifu na jinsi ya kukabiliana na undanganyigu huo. Andika ripoti yenu.

2. Tatizo La kigaidi ni changamoto kubwa sana katika usalama na maendeleo ya kiuchumi hapa nchini. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu sidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachoishia kwa:

..... niliyakumbuka maneno aliyotwambia mwalimu wetu shuleni siku moja. Nilijilaumu si haba na machozi yakanidondoka pukupuku.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 1 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

2 Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

3 Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo uliwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda . Katika msingi huu viwanda vikubwa vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la ajira ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasmia (yenye viwanda vingi) mataifa mengi yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hiyo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huo wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Maswali

a) Kwa nini viwanda ni muhimu? **(alama 2)**

b) Ni nini kiini cha matatizo ya uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea? **(alama 2)**

c) Eleza faida zinazotokana na kuwepo kwa viwanda vidogo vidogo. **(alama 4)**

d) Usambazaji wa viwanda katika maeneo ya mashambani una faida gani? **(alama 4)**

e) Fafanua maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i) Kujasurisha

ii) Amali

iii) Utashi

2. MUHTASARI

Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Watu wengi, wanaamini kwamba kufundisha watoto nyimbo shuleni ni kupoteza wakati unaofaa kwa masomo ya maana. Lakini muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.

Muziki ni kitulizo kikubwa sana cha moyo wa binadamu. Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana. Baadhi ya ujumbe hauwezi kupitishwa kwa njia nyingine ila kwa muziki.

Muziki umetajwa kumsaidia mtoto kwa mambo yafuatayo:

Kuendeza hisia nzuri, za kuburudisha na kuzuzua. Muziki humsaidia mtoto kuweza kukabiliana na tajriba mbaya nazo. Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yake na hivyo kumrejeshea raha tena. Liwazo la muziki ni dhahiri wakati mtoto anapolala pindi anapoimbiwa bembelezi.

Inaaminika pia kwamba muziki unakomaza akili ya mtoto na ni nyenzo muhimu sana katika hafla yake ya kujifanya mambo, hasa kwenye miaka yake ya mapema. Muziki huhitaji umakinifu ili kutambua miondoko na maneno halisi ya wimbo huo na mambo haya humfanya mtoto kuhamisha umakini huu kwenye masomo mengine darasani. Inaaminika pia kwamba kupitia kwa muziki mtoto anaweza kujifunza mbinu ya kukumbuka mambo anayofunzwa masomoni.

Watoto ambao hujifunza muziki mara kwa mara hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na werevu wa mambo mengine kwa jumla. Utafiti

umeonyesha kwamba watu wazima ambao walijifunza muziki kabla wafikishe umri wa miaka 12 huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati kuliko wale ambao hawakujifunza kuimba.

Muziki pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au walio na ulimi mzito wa kuzungumza.

Watoto au watu wazima walio na shida ya kigugumizi huweza kujieleza kwa ufasaha kwa kupitia muziki na jambo hili huboresha kujiamini kwao kwa kibinafsi. Watoto kama hao huweza kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao.

MASWALI

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu. **(maneno 40 – 45) (alama 7)**

MATAYARISHO

NAKALA SAFI

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya nne na ya tano. **(Maneno 45 – 50) (alama 5)**

MATAYARISHO

JIBU

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika sifa mbili mbili bainifu za sauti. **(alama 2)**

i) /e/

ii) /n/

b) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari. **(alama 2)**

i) Hiki ni kitabu cha mwalimu

ii) Hiki ni cha mwalimu

c) Ainisha viambishi na mzizi katika kitenzi **(alama 3)**

d) Hawakunichokoza

e) Bainisha aina za vishazi katika sentensi hii **(alama 2)**

Watoto walioachwa mayatima wamesaidiwa

f) Andika kwa ukubwa na udogo **(alama 4)**

Sahani zote zimepelekwa nyumbani

i) Ukubwa

ii) Udogo.

g) Andika sentensi yakinishi kutokana na sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Utawala mkubwa wa meya haukuzuilika.

h) Andika katika usemi wa taarifa

"Nitawatuza watahiniwa wote watakaopita mtihani mwaka huu". Mwalimu aliwaahidi wazazi. **(alama 3)**

i) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Juma alimchinjia mamake mbuzi mzuri kwa kisu.

j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Wanafunzi waliandikiana barua.

k) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo. **(alama 2)**

(i) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani.

(ii) Wachezaji wote wameingia uwanjani..

k) Eleza matumizi mawili ya kistari kifupi. **(alama 2)**

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. **(alama 4)**

Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri.

m) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Wageni na wenyeji walikimbiliana.

n) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Walimu hao walifanya kazi yao kwa bidii.

o) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo. **(alama 2)**

i) Jaribu

ii) Chuma

p) Kamilisha jedwali **(alama 2)**

Kufanya	Kufanyiwa	Kufanyisha
La		
Fa		

p) Fafanua aina ya hali iliyotumika katika sentensi hii. **(alama 1**

Wanasiasa wengi hulalamika kila mara.

4. ISIMU JAMII

a) Taja mambo manne yanayopelekea kufifia/kufa kwa lugha, **(alama 4)**

b) Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

.....napinga hoja iliyotolewa na waziri wa Finance ya kupiga marufuku matumizi ya plastic bags. Baada ya kumsikiza kwa makini, napenda kumkosoa kwa kudhihirisha kuwa**.....** kulingana na kifungu nambari **.....**

i) Bainisha sajili ya mazungumzo hayo. **(alama 2)**

ii) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza sifa nne za sajili hii kwa mujibu wa kifungu hiki.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 1 PAPER 3

TIME: 2 ½ HOURS

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MAAGIZO

a) Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima
b) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki
c) Usijibu maswali **MAWILI** kutoka sehemu moja.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
JUMLA	80	

SWALI LA LAZIMA

1. **HADITHI FUPI** **ALAMA 20**

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE :

Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda

Mtihani wa Maisha

1. *"..Acha nijiondokee duniani niwaachie wafanisi wafanikie."*
   - **a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **Alama 4**
   - **b)** Taja na ufafanue sifa tatu za msemaji. **Alama 6**
   - **c)** Eleza jinsi maisha ya msemaji yanavyoafiki anwani ya hadithi. **Alama 10**

RIWAYA CHOZI LA HERI : **Assumpta Matei** **ALAMA 20**

2. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri. **Alama 20**

3. *"...liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"*
   - **a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **Alama 4**
   - **b)** Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili.**Alama 6**
   - **c)** Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo''**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. **Alama 10.**

TAMTHILIA KIGOGO : **Pauline Kea** **ALAMA 20**

4. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka." Jadili. **Alama 20**

5. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo
   - ***i)*** Kinaya **Alama 6**
   - ***ii)*** Majazi **Alama 8**
   - ***iii)*** Jazanda **Alama 6**

FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

6. **a)**Eleza **aina** tano za wahusika wa fasihi simulizi. **Alama 10**

b)Eleza sifa za wahusika wa mighani. **Alama 10**

7. a) Eleza namna amabavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji.Toa hoja nne.**Al 8**

b)Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. **Alama 4**

c)Taja viungo vinavyopambanua muundo wa nyimbo katika jami **Alama 4**

d)Andika majukumu manne ya nyimbo katika jamii **Alama 4**

USHAIRI ALAMA 20

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia,namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

Maswali

(a) Shairi hili ni la kimapokeo. Toa sababu mbili **kuunga** kauli hii. **(Alama.2)**

(b) Taja **bahari kuu** ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. **Fafanua**. **(Alama.2)**

(c) Fafanua dhamira ya mshairi. **(Alama.2)**

(d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. **(Alama.2)**

(e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. **(Alama.2)**

(f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. **(Alama.4)**

(g) Mshairi anamaanisha nini anaposema _zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,‘ **(Alama.2)**

(h) Eleza toni ya shairi hili. **(Alama.2)**

(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao.

i) Nitatongoa

ii) Zitapusa. **(Alama.2)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 2 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
i) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Umeteuliwa kama katibu wa kamati iliyochunguza kuzorota kwa elimu katika wilaya yako.

Andika ripoti kuhusu matokeo ya uchunguzi huo.

2. Uvumbuzi wa tarakilishi una athari kubwa katika maisha ya binadamu.

Jadili.

3. Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo ziumiazo.

4. Andika kisa kitakachoanza kwa;

Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho**.....**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 2 PAPER 2

TIME: 2 ¾ HOURS

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

UFAHAMU

(alama 15)

1. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Nimekaa kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao. Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowatengemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali na fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajaribu kuchukua mkopo ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao. hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masualama ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

Maswali.

a) Taja dhamira **mbili** za makala haya. **(alama 2)**

b) Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge. **(alama 2)**

c) Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi? **(alama 2)**

d) Sera za serikali zimesaidia wanawake kivipi? **(alama 3)**

e) Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umaskini kulingana na makala haya. **(alama 3)**

f) Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya **(alama 3)**

i) kutafakari.

ii) kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji.

iii) Riziki.

UFUPISHO (alama 10)

2. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo.***

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuaia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa mwananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idai hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

Maswali.

a) Fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno 50-55. **(alama 8)**

Matayarisho.

Jibu

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 55 - 60.)**(alama 6)**

Matayarisho.

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA. (ALAMA 40)

a) Toa sifa bainifu za sauti /h/ **(alama 3)**

b) Andika sentensi ifuatayo ilete dhana tatu tofauti. **(alama 3)**

Mwaura amekuja.

c) Nyambua kitenzi Lewa katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi.**(al 2)**

d) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. **(alama 2)**

Sitakununulia nguo wala kukutembeza mjini usipomaliza mkate huo.

e) Andika katika umoja. **(alama 2)**

Nyaraka zetu ziliwasilishwa rasmi kwenu na madiwani wa vyama tawala.

f) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. **(alama 2)**

Nimewaleta askari kituoni ili wawalinde wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi.(Anza: Wananchi ...)

g) Iandike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. **(alama 3)**

"Leo nitachimba mtaro uelekeze maji shambani mwangu." mkulima alisema.

h) Tumia neno 'hadi' kama kihusishi cha; **(alama 2)**

i) Wakati

ii) Mahali.

g) Bainisha matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari. **(alama 2)**

Mwalimu anakuita ofisini umweleze ulikoweka kijitabu chake.

i) Bainisha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi hii. **(alama 3)**

Mwanafunzi aliandika insha vizuri.

j) Kanusha bila kutumia 'amba' **(alama 2)**

Nitavaa viatu ambavyo ni safi.

k) Kwa kutolea mifano mitatu, eleza miundo mitatu ya nomino katika ngeli ya A-WA. **(alama 3)**

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale. **(alama 4)**

Watoto wanacheza vizuri ilhali wazazi wakorofi wanawabeza vikali sana.

m) Ainisha mofimu katika sentensi hii. **(alama 3)**

Aliyemletea.

n) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

o) Wapatie nafasi wabunge wale.

Unda kivumishi kutokana na kitenzi dhulumu na utungie sentensi. **(alama 2)**

4. ISIMU JAMII. **(alama 10)**

a) Lugha ya Kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Taja matano na kuyaeleza. **(alama 5)**

b) Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya. **(alama 5)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 2 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3 (FASIHI)

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) *Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali manne pekee.*
d) *Swali la **kwanza** ni la lazima.*
e) *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.*
f) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili.*
g) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SWALI LA LAZIMA.

1. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini.Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba.Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi.Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza.Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura.Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata.Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

Maswali

(a) Tambua utanzu na kijipera chake. **(al.2)**

(b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. **(al.2)**

(c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki**.** **(al.5)**

(d) Eleza sifa za kifungu hiki. **(al.5)**

(e) Eleza umuhimu wa fomyula:

(i) Kutanguliza **(al.3)**

(ii) Kuhitimisha **(al.3)**

TAMTHILIA ; KIGOGO NA TIMOTHY AREGE

2. Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al.4)**

(b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki**.** **(al.4)**

(c) Eleza matatizo yanayoikumba safari inayorejelewa**.** **(al.12)**

3. Eleza nafasi ya mwanamke katika jamii ya kigogo. **(al.20)**

RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASHUMTA K. MATEI

4. Matatizo mengi yanayowakumba wahusika wengi katika riwaya hii ni mwiba wa kujidunga. Jadili **(al.20)**

5. Kwa kurejelea riwaya hii, fafanua mbinu zifuatazo. **(al.20)**

(i) Kinaya

(ii) Mbinu rejeshi

(iii) Sadfa

(iv) Jazanda

HADITHI FUPI: TUMBO LISILISHIBA.

6. Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo na shogake dada ana ndevu fafanua changamoto zinazowakumba vijana**.** **(al.20)**

7. ***Mame Bakari***

"Una nini ? Umeshtuka mwanangu ! Unaogopa? Unaogopa nini?"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(al.4)**

(b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo. **(al.2)**

(c) Eleza sifa za mrejelewa**.** **(al.6)**

(d) Eleza umuhimu wa msemaji**.** **(al.4)**

(e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. **(al.1)**

(f) Fafanua maudhui katika swali la (***e)*** kwa kurejelea hadithi nzima. **(al.3)**

8. USHAIRI.

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Sinusubuwe akili, nakusihi e mwandani
Afiya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini
Sisi tokea azali, twende zetu mizimuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
Dawa yake ni subili, au zogo huauni
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini.
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Waambiwa damu, kalili ndugu msaidieni
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wamajano na wa kijani
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi mlangoni?

MASWALI.

a) Lipe shairi hii anwani mwafaka. **(al.1)**

b) Toa sababu zinazofanya mshairi kutokana kwenda hospitali. **(al.3)**

c) Andika ubeti wanne kwa lugha ya nathari/ tutumbi. **(al.4)**

d) Taja bahari mbili zilizotumika katika shairi hili. **(al.2)**

e) Tambua nafsineni katika shairi hili. **(al.1)**

f) Tambua toni ya shairi hili. **(al.1)**

g) Eleza muundo wa shairi hili. **(al.4)**

h) Fafanua uhuru wa mshairi unavyojitokeza katika shairi hili**.** **(al.2)**

i) Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili.

(al.2)

(i) Dhalili

(ii) Azali

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 3 PAPER 1

TIME: 2 ¾ HOURS

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
i) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. **Insha ya lazima**

Andika dayolojia kati ya katibu wa usalama wa ndani na waandishi wa habari kuhusu jinsi ya kuzuia uhalifu nchini

2. Sheria zinazombagua mwanaume na kumpendelea mwanamke zinafaa kutupiliwa mbali. Fafanua

3. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya

5. Lo, yaliyotendeka katika makazi ya jirani yetu usiku huo yalikuwa ya kutisha sana. Kumbe watu wamegeuka hayawani! Hayawani .....

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 3 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

2 Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

3 Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU

Shule yangu ya upili

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea. Nikiwa sitetereki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe. Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuaamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Runda. Wakati wa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.

Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana, kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati. Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe. Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika. Alfajiri, dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni. Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu. Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema, safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha, safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango. Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika lango la shule ya kitaifa!

Tulipotia ozi tu!!....jamani.....jamani nikafa moyo. Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu, nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini. Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kujali kuvikarabati. Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopita na yalistahili kuitwa makafadhi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano. Asiye na wake ana Mungu, nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto langu. Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walioniona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa. Nikasajiliwa!

Sikujua, hakika sikujua, sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi. Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hata kushindwa kununua rangi ya kupaka viatu hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani? Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia. Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura nichafukwe na moyo, makapi ya mboga na uchafu

usioelezeka ulinikumba, kisha nikapewa kisahani cha plastiki na kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa. Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanihisi nimpe chote na kukimaliza fyu. Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi.

Baada ya mlo 'rojo rojo', tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu. Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala, kimombo chake kilinishangaza, hasa matamshi yake yalipungukiwa na kudhirisha athari za lugha ya asili. Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu. Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wepi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo, akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu, sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi. Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu!

Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la. Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada au la, ndio, hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao, labda hawakuyatambua.

Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza. Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga. Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane, nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu!

Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

Maswali

a) Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo dhabiti **(alama 2)**

b) Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili **(alama 3)**

c) Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili. **(alama 3)**

d) Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili **(alama 3)**

e) Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu. **(alama 2)**

f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. **(alama 3)**

i) alimstahi

ii) kughairi

iii) kunighasi

MUHTASARI

Tulipigwa na butwaa kwa kupokea habari kuhusu mauaji ya wasafiri 28 waliouwawa kikatili huko Mandera na kabla kuwasidikiza makaburini wengine waliokuwa 40 wakijitafutia riziki katika chimbo la mawe kuko huko, wakaangamizwa. Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelezwa kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini. Vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Iwapo mbunge anayelindwa na askari wawili atawauwa, je wananchi wa kawaida watakosa kumuua? Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao imedumishwa. Polisi nao wanashambuliwa huko Kapendo na kumiminiwa marisasi wasiweze kujikinga tukabaki kuwazika licha ya umri wao mdogo ili kukabiliana na tatizo hili, polisi wakaamua kusaka wahalifu. Lakini cha kusikitisha kuwa mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa hii ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha Wakenya kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majajusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu

kutoka kwa raia. Ni ajabu kuwa sisi tunaelekeza kidole cha lawama kwa serikali ilhali wahalifu hawa tunaishi nao katika mitaa tunakoishi, viongozi wapinzani wasipinge mikakati yoyote ya serikali kama vile mpango wa nyumba kumi kisa na maana si wazo lao. Iwapo hawapendezwi na mpango kama huo waibuke na mbinu badala tuzijaribu. Suala la **'**serikali ingilie kati**'** hata bwana mlevi anapochapwa na mkewe lisukumwe katika kaburi la sahau.

Maswali

a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi?

Tumia maneno 80 **(alama 7, 1 utiririko)**

Matayarisho

Nakala safi

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho

(alama 6, 1 utiririko)

Matayarisho

nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Badilisha vitenzi hivi viwe katika hali ya kuamuru **(alama 2)**

1) kuleta

2) kuja

b) Tumia kiungo 'na' katika sentensi kuonyesha: **(alama 2)**

1) Ufupisho wa nafsi ya kwanza umoja fulani

2) kihusishi kuonyesha aliyetenda jambo fulani

c) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

1) Mwalimu amesema ya kwamba watoto wengi wamekuwa wahuni.

2) Ikiwa nitamwona mama sokoni, nitamweleza kila kitu

d) Ainisha viungo vya kisarufi katika sentensi hii **(alama 3)**

Alani

e) Tumia kitenzi **'cha'** katika kauli ya kutendesha katika sentensi **(alama 2)**

f) Tumia kiambishi ngali katika sentesi kuonyesha hali ya kuendelea **(alama 2)**

g) Tofautisha kwa kueleza maana ya istilahi hizi: **(alama 2)**

ghuna

si ghuna

h) Changanua sentensi kwa njia ya matawi **(alama 4)**

Yeye na mama yule si watu wazuri sana

i) Eleza sifa bainifu za sauti zifuatazo **(alama 4)**

i) /I/

ii) /ch/

j) Tumia kielezi cha namna kiigizi katika sentensi **(alama 2)**

k) Andika sentensi hii upya katika **usemi halisi** **(alama 2)**

Mwanafunzi alimsihi mwalimu asimwadhibu wakati huo

l) Onyesha chagizo katika sentensi hii **(alama 2)**

Mtoto alikula kwa utaratibu jana jioni

m) Tambua na uainishe shamirisho katika sentensi hii **(alama 3)**

Hamu amemwandikia mwalimu riwaya kwa kalamu

n) Unda vitenzi kutoka kwa maneno haya kisha uyatumie katika sentensi yakiwa katika hali hiyo ya kitenzi **(alama 2)**

i) Marashi

ii) bora

o) Tofautisha kati ya vivumishi hivi kwa kueleza maana ya kila kimojawapo**(al 2)**

i) -ingine

ii) -ingineo

p) Sahihisha makosa katika sentensi hii **(alama 2)**

Mtoto mgani mwenye kupiga kelele darasani

q) Tumia maneno haya katika sentensi ili kuyatofautisha **(alama 2)**

shoka

choka

shoga

ISIMU JAMII

Nani kuku.....? Sosi poa leo ..... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka kumi..... Ng'ombe je? nani? .....nani!... Ni wewe..... poa basi naja.....

a) Ni sajili gani inayorejelewa hapo juu? **(alama 2)**

b) Andika sifa za sajili hii ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu **(alama 8)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 3 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili.
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
h) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU A: RIWAYA YA CHOZI LA HERI.

"Tangu lini mavi ya kale yakaacha kunuka?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

(b) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo hili **(alama 2)**

(c) Kwa kutumia hoja sita eleza mavi yanayozungumziwa katika dondoo hili. **(al. 6)**

(d) Kwa kutumia hoja nane eleza sifa nane za mrejelewa. **(alama 8)**

SEHEMU B: TAMTHILIA:KIGOGO NA PAULINE KEA.

2. "Ukitaka kukula asali kaa na nyuki!"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Bainisha mbinu zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Eleza jinsi wahusika hawa walivyofaidi kutokana na kukaa na nyuki. **(al 2)**

(i) Chopi

(ii) Kenga

(iii) Ngurumu

(iv) Mamapima

Au

3. Eleza jinsi mwandishi wa Tamthilia hii ya Kigogo alivyotumia mbinu ya majazi. **(alama 20)**

SEHEMU C. USHAIRI.

Fanya swali la 4 au 5

4. Sinisumbue akili, nakusihi w mwandani,
Afya yangu dhalili, mno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisi tokea azali, twende zetu misumuni,
Nifyateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu za irijali, Mkuyati uamini,
Kaafuri pia kali, dawaya ndwele Fulani,

Niftwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zonto huanoni,
Zabadili pia sahali, kwa maradhi yako ndani,
Au kwenda wasili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa siko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Daktari k'ona mwili, tanenea kensa tumboni,
Visu sitiwe makali, tayari kwa pirisheni,
Ukatwe kama fagili, tumbo nyangwe na maini,
Niftwateni sipitali, na dawa siko nyumbani?

Japo maradhi dhalili, kutenguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani,
Waambiwa dmu katili, ndugu msaidieni,
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yakata vitu thamani,
Utete huku wawili, wa manjano na kijani,
Matunda pia asali, vitu vya shimoni,
Nifwateni sipitali, na dawa zi langoni?

Maswali:

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. **(alama 2)**

(b) Eleza umbo la shairi hili. **(alama 4)**

(c) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika shairi hili? **(alama 2)**

(d) Onyesha jinsi uhuru wa utunzi ulivyodhihirishwa katika shairi hili **(alama 3)**

(e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya tutumbi/nathari. **(alama 4)**

(f) Tambua mbinuya utunzi inayobainika katika mshororo wa mwishow a kila ubeti. **(alama 2)**

(g) Onyesha maana ya maneno yanyofuata kama yalivyotumiwa na mshairi. **(al. 3**

(i) Dhalili

(ii) Kensa

(iii) Ndwele

5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali. (alama 20)

Barabara.

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena,
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka".

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendeleee kujitahidi kw akila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua,
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

(Timothy Arege)

Maswali:

(a) Taja na ueleze aina ya shairi hili. **(alama 2)**

(b) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**

(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. **(alama 2)**

(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. **(alama 3)**

- **(i)** Tanakali za sauti
- **(ii)** mbinu rejeshi
- **(iii)** Taswira

(e) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika shairi. **(alama 2)**

(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. **(alama 4)**

(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. **(alama 2)**

(h) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. **(alama 3)**

- **(i)** Kuruba
- **(ii)** siha
- **(iii)** machweo

SEHEMU D.

6. HADITHI FUPI.

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE:

"Umaskini ndio chanzo cha matatizo ya kijamii"

Kwa kuzingatia hadithi zifuatazo nne katika diwani ya Tumbo lisiloshiba na Hadithi nyingine, thibitisha ukweli wa kauli hii.

(i) Tumbo lisiloshiba

(ii) Mapenzi ya kifaurongo

(iii) Ndoto ya mashaka

(iv) mkubwa

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

7. (a) (i) Eleza tofauti ya ngoma na ngomezi. **(alama 2)**

(ii) Taja aina nne za ngomezi za kisasa **(alama 4)**

(b) (i) Mivigha ni nini? **(alama 2)**

(ii) Eleza sifa zozote nne za miviga **(alama 4)**

(c) Fafanua majukumu ya michezo ya watoto (chekechea) **(alama 8)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 4 PAPER 1

TIME: 2 ¾ HOURS

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

MUDA: SAA 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
i) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. INSHA YA LAZIMA

Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa na mkuu wa wilaya kujadili kuhusu madhara ya pombe haramu na mbinu za kuangamiza pombe hiyo wilayani. Andika ripoti ya kamati hiyo.

2. Unyanyasaji wa kijinsia umekithiri katika jamii yetu ya leo. Thibitisha.

3. Sikio la kufa halisikii dawa.

4. Andika insha itakayomalizikia na:

..... Wazima moto waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatokea. Maajabu yaliyoje!

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 4 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

MAAGIZO

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya uchaguzi kukoka kuendeleza uchaguzi kwa njia inayostahili. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

Hivi sasa wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya wakenya vimeshamiri na kupaaza sauti vikilalamikia kukosa makazi, lishe na ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya 'wenyeji' kuwatimua 'wageni' na damu kumwagika.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbizi kutoka nchi jirani zinazokubwa na vita vya wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu; ukabila na tamaa ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyama vikuu vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila kila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine, viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wameamua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya Wakenya ni wakimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na shirika la msalaba mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa lakini kuna tetezi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao.

Matukio kama haya hayastahili kutukia asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao **aali** la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikizia mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu undugu na utaifa. Fauka ya haya masuala yanayohusiana na hatimiliki za ardhi yanafaa kutadarukiwa kwa dhati.

Maswali

a) Toa anwani mwafaka kwa makala haya. **(alama 1)**

b) Taja madhara **manne** ya ukabila. **(alama 2)**

c) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekubwa na changamoto gani? **(alama 2)**

d) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. **(alama 2)**

e) Mwandishi anatoa mapendekezo gani ya kutatua tatizo hili la ukabila.**(alama 4)**

f) Eleza kinaya cha maisha ya wakenya kwa sasa. **(alama 2)**

h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu.

(alama 2)

i) Mawio -

ii) Tandarakiwa kwa dhati

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Africa kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya waoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la ukimwi limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishi kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. Ukimwi umezifanya familia nyingi pia kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kusalisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa umoja wa Africa hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto nchi za Africa hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo, ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

Maswali

a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza.

(maneno 45 - 50)(al 6, 1 ya mtiririko

b) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho

(maneno 50 - 55)(Alama 7, 1 ya mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja vikwamizo **viwili** ambavyo ni kosonanti hafifu **(alama 2)**

b) Sentensi hizi ni za aina gani? **(alama 2)**

i) Uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya

ii) Naomba uwaite wanafunzi wale

c) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye nomino zifuatazo **(alama 2)**

i) meza

ii) Maneno

d) Nomino 'Risasi' iko katika ngeli gani? **(alama 1)**

e) Andika sentensi ifuaayo katika hali yakinishi **(alama 2)**

Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama.

f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya alama za mtajo**.(alama 2)**

g) Andika katika wakati ujao hali timilifu **(alama 2)**

Wanafunzi walifanya mtihani wa mwigo

h) Tunga sentensi mwafaka ukitumia kielezi cha:- **(alama 2)**

i) Namna kiigizi

ii) Cha mahali

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. **(alama 4)**

Mwanasiasa mwingine amepoteza kiti chake cha ubunge.

j) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi ndi-**(alama 2)**

k) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii. **(alama 2)**

Kuimba ambako kutavutia kutashinda tuzo

l) Tunga sentensi yenye fungu tenzi lenye muundo ufuatao **(alama 2)**

tS + T + N

m) Andika kwa usemi wa taarifa **(alama 2)**

Mama watoto aliuliza, "mbona mnajikunyata kama mayatima".

n) Badilisha vitenzi vifuatavyo viwe katika hali ya kutendeka. **(alama 2)**

i) kwea

ii) dhuru

o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kihisishi cha kukataa. **(alama 2)**

p) Bainisha aina za nomino zilizotumika katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Kikosi cha askari kiliabiri ndege hadi ujerumani

q) Kanusha kwa umoja **(alama 2)**

Mkilia mtapewa maziwa

r) Andika kwa udogo hali ya wingi **(alama 2)**

Ngoma imepigwa na msichana yule mpaka imepasuka.

s) Unda kitenzi kutokana na nomino ifuatayo. **(alama 1)**

Taifa

4. ISIMU JAMII (AL 10)

Eleza makosa matano yanayoweza kutokea wakati wa mazungumzo. **(alama 10)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 4 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
g) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A.

SWALI LA LAZIMA

TUMBO LISILOSHIBA na hadithi nyingine (wahariri: A. Chokocho na D. Kayanda)

1. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, 'Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.' Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. **(alama 20)**

SEHEMU B.

TAMTHILIA: Kigogo Puline Kea

2. **"**Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba….kuturejesha ….hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b. Kwa kumrejelea mzungumzaji wa maneno haya, bainisha unafiki katika kauli hii. **(alama 16)**

3. Eleza jinsi mbinu ya taharuki ilivyotumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. **(alama 20)**

SEHEMU D. RIWAYA.

CHOZI LA HERI NA *Assumpta Matei*

4. Jadili maudhui ya '**migogoro'** katika riwaya ya Chozi la Kheri. **(al 20)**

5. " …alinionya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama…"
   - **a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
   - **b)** Fafanua sifa nne za anayehusishwa na maneno haya. **(al 4)**
   - **c)** Onyesha namna ukiukaji wa haki za watoto unavyotokea katika riwaya hii. **(alama 12)**

6. SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI

a) Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi. **(alama6)**

b) Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi.**(alama6)**

c) Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti. **(alama 2)**

d) Tambua dhana zinazotokana na maelezo haya.

i. Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla**?** **(alama1)**

ii. Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani? **(alama 1)**

iii. Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje? **(alama 1)**

iv. Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwa **(alama 1)**

v. Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake**?(alama 1)**

vi. Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili**.** **(alama 1)**

SEHEMU YA E. USHAIRI

7. SHAIRI A

MWANA
1. Kwani mamangu u ng'ombe, au u punda wa dobi?
Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

MAMA
2. Nong'ona mwana nong'ona, sitafute angamiyo
Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
Kwani kelele kunena, huyataki maishiyo?
Hilo nakwambia.

MWANA
3. Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo

Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo
Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni
Nini yako matulubu, kulima hadi jioni?
Na jembe ukidhurubu, ukilitua guguni
Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani
Hajali hakuthamini, wala haoni huzuni
Mwisho wa haya ni nini, ewe mama wa imani?
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
Ukichelewa vituko, baba anakutandika
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
Kiishapo u mbioni, wapita kupokapoka
Urudi nje mekoni, uanze kushughulika
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo

MAMA
Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
Ninaanza kujipinda, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia

MASWALI

a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili. **(alama 2)**

b) Shairi hili ni la aina gani ? Toa ithibati. **(alama 2)**

c) Yataje mambo yoyote matano anayoyalalamikia mwana. **(alama 5)**

d) Eleza kanuni zilizotumika kusarifu ubeti wa tatu. **(alama 5)**

e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. **(alama 4)**

f) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika shairi hili.

(i) jaza **(alama 1)**

(ii) muhibu **(alama 1)**

AU

8. SHAIRI B

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

1. Punda kalibebe gari, gari limebeba punda
Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda
Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda.
Kinyume mbele

2. Saramala ahubiri, muhunzi tiba apenda
Mganga anaabiri, baharini anakwenda
Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda
Mtazame askari, akazakaza kitanda,
Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
Kinyume mbele

4. Apakasa daktari, ukili anaupinda
Saveya kawa jabari, mawe anafundafunda,
Hazini wa utajiri, mali yote aiponda,
Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda
Fahali hawasimami, wanene waliishakonda
Walojitia utemi, maisha yamewavunda
Kinyume mbele

6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
Tele haitakadari, huvia tulivyopanda
Mipango imehajiri, la kunyooka hupinda
Kinyume mbele

MASWALI

a) Mtunzi alikuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? ***(alama 3)***

b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. ***(alama 4)***

c) Eleza namna mtunzi alivyoutumia uhuru wake. ***(alama 5)***

d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? ***(alama 2)***

e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari. **(alama 4)**

f) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**

mwisho

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 5 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
i) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

1. **Lazima**

Siku za hivi karibuni imekuwa kawaida kwa wanafunzi wa shule ya upili ya Matumaini kusokotwa na tumbo baada ya kila mlo. Ukiwa katibu wa Baraza la Wanafunzi matokeo ya uchunguzi wenu.

2. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
Atanguliaye kisimani hunywa maji maenge

3. Matokeo mema ya mtihani wa katika shule yoyote ya humu nchini hutegemea juhudi za mwalimu mkuu pekee Jadili.

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo:
...mwishowe nilikuja kungamua kwamba jitihada za wenzangu ndizo zilizonisaidia kuvuka daraja hiyo.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 5 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

2 Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

3 Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

UFAHAMU (Alama15)

Soma makala yafuatao kisha ujibu maswali yanayofuata.

Tunapoakisi hatua ambayo mfumo wa kiteknohama umepiga misamba, kizazi cha vichakazi (facebook) kimetoweka na kupisha kile cha kututumiwa (GMO). Sidhalilishi hivi vikembe na vijikembe vya kututumuliwa japo kunao wenye falfasa hasi kuhusu vikembe hivi. Vijetegemeo mji wao ja waso haya.Hivi vya kutitimuliwa vina mitindo anuai ya kujinakia.Kama wewe si kufu au lahiki yao basi wewe jua bayana kuwa umepitwa na wakati. Utembeapo katika vitongoji vya janibu hizi si Gitau hadi Kaanwa, si Thuchi hadi Mutuati...sisemi Mukothima, utapatana na vikembe HIVI VYA KUTUTUMULIWA. Barobaro hujivika magwanda yanayoonekana kama yatabambuka wakati wowote na kuacha wazi sehemu tunazotegemea.

Vijembe navyo huwa vimejisetiri nusu kwa vijigwanda ambavyo vimeundwa kutoka kwenye shashi. Wafahamu shashi?Kile kitambaa kidogo cha kupangusia pua. Japo mimi vizazi hivi huviona maridadi na anisi, ni yakini kwamba maadili yamewapaa kabisa. Maghulamu wa kukutumuliwa hutembea kwa miondoko au kwa kudakia ukipenda. Zamani nikiwa mdogo tulivaa kaptura na shati za kawaida.Tulijinakia kuchezea matope huku tukivaa nguo safi siku ya Dominika pekee.

Vikembe vya kututumuliwa daima vina vidubwasha maskioni vikiburudika kwa mahadhi ya miziki kutoka kwenye simu zao za ruhunu. Hata kikutane na nani au nani sharti ampishe njia.Enzi zetu mwalimu hakuwa akifanya mambo mengine kama vile kula aina fulani ya chakula sisemi hata kwenda haja. Ukipatana naye njiani wee! Sharti utafute mahali ujifiche mpaka mwalimu apite.Vikembe vya kututumuliwa huwa tunaviheshimu sana. Mara nyingi vitakuona vipi na huku vikembe na vijikembe hutembea huku vimepatikana kama mwanakima na mamake. Waso haya wana mji wao.

Ukikutana nvyo njiani utatamani kurudisha saa yako ya maisha nyuma kidogo. Lakini ndugu, ujajani moshi, ukienda .. Hubagui baina ya vikembe na vijikembe kwani wote vipuli vimebanwa katika sikio moja na kama si moja kijikembe cha kututumuliwa huwa na kipuli kirefu kifikiapo hadi begani.Kijikembe hutembea huku kimesetiri miguu yake kwa jumu yake kwa jumu ambazo zimefika hadi kwenye goti. Na visigino je? Yuatembeahuku akihofu ardhi isibonyee au kuseteka./

Enzi zetu kila baada ya shughuli za shule jioni tulikuta faradhi za kila nui zatusubiri. Mojawapoilikuwa kuwapeleka mifugo malishoni. Kizungumkuti kilikuwa pale ambapo katika michezo yetu ya vijana, ng'ombe wataishia katika shamba la jirani. Jioni hiyo sharti uyatayarishe sisemi makalio kwa utovu wa tafsida Lakini mijeledi itazuru hapo si katiyi.

Vile vikembe vyetu vya kututumuliwa vitakuwa pengine kwenye runinga au kwenye simu zao za rununu na wakati mwingine vimepakata vipakatalishi huku vikibovya vidude hapa na pale. Kila shughuli yao huwa ya mwendo wa pole pole havina mchapuo. Vinyonge hivi si kama vya enzi ya mababu zetu ambao walikuwa wakichapa mpira juu na kuketi kunusa ugoro huku wakisubiri mpira urudi ndiposa waendelee na mchezo wao.

Vikembe vya kutumuliwa huupisha tu na kikiteleza na kuanguka kidogo basi, mchezo umekoma hadi kipelekwe si zahanatini Lakini katika hospitali kuu ya daraja latano.

Kila jumapili jirani yangu alikuwa na zamu ya kushughulikia kichwa change kwa wembe wake. Hakuwa na shufaka au huruma ukipenda. Kichwa kilibaki kama kupe. Usishtuke kuviona vikembe vya kututumuliwa vichwa vyao vina ukwasi wa nywele si kipilipili bali kama za Bob Marley. Naona kana kwamba siku hizi kunz uhaba wa vinyoleo

Sisemi kizazi kimetukinai, hata chembe. Ni kwa kiteule kwa hivyo tusikipurukushe au kukinyanyapaa. Kila uchao lawana zaradidiwa kuhusu kizazi hiki. Haya ni mambo mazito ja jabali na hivyo basi kinachobaki ni kukihusisha katika ushaui na nasaha. La sivyo sisi wenyewe ndio tutakuja kulio kilio cha mbwa mdomo juu.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 2)**

b) 'Kizazi chetu kimekosa maadili.' **(alama 3)**

Thibitisha kwa mujibu wa taarifa hii.

c) Eleza tofauti nne ambazo mwandishi ameangazia kati ya kizazi cha zamani na kile cha kisasa. **(alama 4)**

d) Mwandishi anamaanisha nini kwa : **(alama 3)**

- ***i.*** ...umepitwa na wakati
- ***ii.*** ...vimeundwa kutoka kwenye shashi
- ***iii.*** mijiledi itazuru hapo si katiti

e) Eleza maana za maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. **(alama 3)**

- ***i.*** kujinaki
- ***ii.*** faradhi
- ***iii.*** tusikipurukushe

2. SEHEMU B: UFUPISHO(ALAMA 15)

Inaridhisha kuyasikia mengi kuhusu mikakati ambayo serikali imeanzisha kuimarisha maendeleo ya nchi.Ni kweli kuwa maendeleo huhitajika kuonyesha mafanikio ya nchi ili kumaliza umaskini nchini.Ni juzi tu serikali imeanzisha ujenzi wa reli ambao umeibua malumbano mengi pamoja na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta ukiwa miongoni mwa miradi mengine mingi.

Kuna mipango kabambe ya kuwezesha usafiri wa maji uimarike zaidi katika mto Nile ili manufaa yake pia yaonekane katika eneo la Afrika mashariki sio tu Misri.

Ustawi wa taifa pia umelengwa kwa kupigia debe swala la pesa mashinani ili serikali za gatuzi ziweze kufadhili miradi moja kwa moja bila kutegemea serikali kuu.Na Ikiwa ugatuzi huu utafaulu basi vijana na wanawake washugulikiwe kwa kuwapa mikopo ya kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Maendeleo hayawezi kuimarika bila ujenzi na upanuzi a barabara ili kukuza teknolojia ya mawasiliano.Jambo hili litarahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Elimu pia ni kigezo muhimu na msingi thabiti wa kuega uchumi kwa kila nchi.Katika mabara yalioendelea asilimia kubwa ya wnanchi huwa na kiwango cha juu cha elimu.Kwa hivyo ni jambo muhimu kwa serikali kutoa elimu ya bure katika shule za msingi hadi shule za upili.Pia kilimo kipanuliwe kwa kutumia mbinu za kisasa na teknolojia mpya iwezeshe kwa hali na mali mashambani ili kuwaajiri watu wengi katika sekta hiyo.

Azma na matumaini ya kila nchi kuendelea hukabwq na matatizo kwa kuwa Fedha zinazohitajika zinashinda hata bajeti y mwaka mzima ya nchi hizo.Kuna uhaba mkubwa wa wataalamu mbalimbali wenye ujuzi wa kufaa katika sekta nyingi hapa nchini.

Pamoja na kuweko kwa viongozi wenye matumbo makubwa ambao humimina Fedha zenye manufaa kwa wananchi,kuna ukosefu wa vifaa vya kisasa vinavyorahisisha utenda kazi.Vikiwepo huwa duni kulingana na viwango vya maendeleo.

Kuna pengo kubwa sana kati ya matajiri na maskini hivi kwamba itachukua muda kuyashawishi matabaka haya mawili.Takwimu sahihi ya mahitaji ya watu katika maeneo fulani yahitajika ili serikali iweze kusambaza miradi kulingana na jinsi eneo lilivyo.Wamiliki ardhi kubwa wamekuwa na mzizi iliyokita kwenye ulingo wakisiasa hivi kwamba ni vugumu na hatari kugusia suala la umiliki wa ardhi.

a) Ni juhudi zipi zilitiliwa maanani kuimarisha uchumi? **(maneno 55)**
(alama 6,1 ya utiririko)

Matayarisho

jibu

b) Kwa maneno yasiyozidi 55 fupisha aya tatu za mwisho.**(alama 7, 1 ya utiririko)**

Matayarisho

Jibu

3. SEHEMU YA C : MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika mifano minne ya vitenzi vya silabi moja katika ya kutendesha.**(alama 2)**

b) Unda sentesi yenye muundo ufuatao : **(alama 2)**

KN(N+V),KT(t+ V+E)

c) Taja sifa inayotofautisha sauti / ny/na/ng/ **(alama 2)**

d) Ainisha vihusishi katika sentensihii :

Tulichakura tarakilishi ya mwalimu iliyokuwa kando ya dawati baada ya mtihani kukamilika. **(alama 3)**

e) Tumia kiunganishi seuze / sembuse katika sentensi. **(alama 2)**

f) Eleza maana tatu za sentensi hii.

Chakula kingine kimeliwa na wageni. **(alama 3)**

g) Ainisha vitenzi katika sentensi hii.

Hawa ndio wageni tuliokuwa tukingojea kwa hamu. **(alama 2)**

h) Hizi ni mofimu za aina gani? **(alama 3)**

Kiwavi
Miwani
Karatasi

i) Akifisha

Toka nje au niku nyanya akaamuru murithi **(alama 3)**

j) Changanua kwa kutumia vishale.

Swali hilo lilikuwa rahisi sana. **(alama 4)**

k) Yakinisha

Chakula hakiko tayari hivyo wageni wasinawe mikono. **(alama 2)**

l) Ainisha vishazi katika sentensi hii.

Kama nitamkuta nyumbani nitamshauri asome kwa bidii. **(alama 3)**

Tunga sentensi ya neno moja yenye sehemu zifuatazo : **(alama 3)**

m)
Kikanushi
Hali timilifu
Mtendewa
Kitenzi cha silabi moja
Kauli ya kutendesha
Kiishio

n) Andika katika usemi wa taarifa :

“Mkishinda timu hii leo nitamtuza.”Mkufunzi akatwambia. **(alama 3)**

o) Tambua yambwa na ueleze ni za aina gani.

Wazazi waliwanunulia wanafunzi bora zawadi nyingi kwa hundi. **(alama 2)**

p) Nyambua neno hili katika kauli ya kutendesha. **(alama 1)**

Jua

4. SEHEMU D : <u>ISIMU JAMII</u> (ALAMA 10)

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali

Anachukua ile ngoma kijana Rooney,

Kwake chicharito...anachenga moja , mbili

Hatari! Hatari! Hatari kwenye lango..

a) Hii ni sajili gani? **(alama 2)**

b) Eleza sifa nane za sajilli hii. **(alama 8)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 5 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
g) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU A(SWALI LA LAZIMA)

A: USHAIRI

.Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu,ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Maswali

(a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. **(alama 1)**

(b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi**.** **(alama 2)**

(c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi. **(alama 2)**

(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. **(alama 4)**

(e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. **(alama 2)**

(f) Eleza umbo la shairi hili. **(alama 4)**

(g) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 1)**

(h) Fafanua dhamira ya mshairi. **(alama 2)**

(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. **(alama 2)**

(i) Malofa:

(ii) Udubu:

SEHEMU YA B:

RIWAYA: CHOZI LA HERI – ASSUMPTA K. MATEI

Jibu swali la 2 au la 3

2. "Lakini itakuaje historical injustice, nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Taja na utpe mifano ya mbinu za sanaa zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya**.** **(alama 2)**

(d) Ni mambo gani yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho. **(al 10)**

3. Uozo wa maadili ya jamii umekithiri katika Riwaya ya Chozi la heri, Fafanua ukweli wa usemi huu. **(alama 20)**

SEHEMU C:

TAMTHILIA: KIGOGO – PAULINE KEA

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Asante ya punda kweli ni mateke. Sikujua ungekuja kunihangaisha……"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

(b) Onyesha jinsi msemewa anamhangaisha msemaji. **(alama 2)**

(c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha ukweli wa methali "Asante ya punda ni mateke. **(alama 14)**

5. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya Kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi. **(alama 20)**

(a) Jazanda

(b) Majazi

SEHEMU D;

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE.

6.Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya 'Tumbo Lisiloshiba na hadithi Nyingine',

jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi**.** **(alama 20)**

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ndimi Nguli, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania gozi kusakata nami.

Maswali

(a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 2)**

(b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. **(alama 10)**

(c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 8)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 6 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
g) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Baada ya kutafitia mazingira nchini, kumeibuka tata kadhaa za kimazingira ambazo zinaathiri uzalishaji wa vyakula. Andika ripoti ukibainisha tata hizo na upendekeze namna zinavyoweza kusuluhishwa.

2. Nchi ya Kenya imekumbwa na janga la njaa kwa miaka mingi. Jadili athari za janga hili nchini

3. Andika kisa kitakachoafiki ukweli wa methali ;**Udandao ndio ukubwagao.**

4. Bahari ilikuwa imetulia tuli.Tulikuwa na furaha tele baada ya kufanikiwa kuvua samaki wengi ajabu. Kwa umbali tuliweza kuona ufuo. Ghafla, mashua yetu ikaanza kuyumba.....Endeleza usimulizi huu.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 6 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……

SCHOOL…….. SIGN 102/2

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo.

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani.Kunayo saratani ya ngozi — vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitishia hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung ‘olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo.
Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na

kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kingo zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na ,ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na Si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

MASWALI

(a) Yape makala haya kichwa **(alama 2)**

(b) Mbali na athari kwa uzazi wa kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. **(alama 3)**

(c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(alama 4)**

(d) Je,ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu **(alama 2)**

(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alama 3)**

(f) Eleze maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa.

(i) Gandwa

(ii) Tunguka

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

RIPOTI YA SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE

Wakati wa kuzaliwa, kiwiliwili cha mtoto wa kike huwa kimekomaa vizuri zaidi kuliko cha wavulana aidha wao huwa na mfumo wa kinga ya kimwili bora kushinda wa watoto wa kiume.

Kwa sababu hii watoto wengi wa kiume huaga dunia kuliko wale wa kike kabla ya kutimiza miaka mitano.Kulingana na Benki ya Ulimwengu, takriban wavulana 112 kati ya 1000 huaga kabla ya kufikisha miaka mitano kinyume na wasichana 95 tu ambao huaga kabla ya kufikisha miaka mitano.

Hali hii ya watoto wa kike kuwa bora kuliko ya wale wa kiume hubadilika wanapofikia umri wa miaka 6. Uchunguzi wa kiuchumi unaonyesha kuwa mwaka 2010 takriban wavulana 736,700 walijiunga na darasa la kwanza huku wasichana 731,800 pekee wakijiunga na darasa la kwanza.

Kufikia mwisho wa darasa la 8, tofauti hii ilibainika zaidi ambapo asilimia 71 tu ya wasichana ndiyo iliyohitimisha elimu ya shule ya msingi ikilinganishwa na asilimia 74 ya wavulana hapa nchini Kenya.

Asilimia 43 pekee ya wasichana walijiunga na shule ya upili huku ile ya wavula na ikiwa 47.Asilimia 64 ya wasio na elimu nchini Kenya ni wasichana.

Si katika elimu tu ambapo wanawake hawajaimarika bali hata kiafya.Nchi ya Kenya bado ina visa vingi vya vifo vya wanawake wakati wa kujifungua duniani. Kwa kila wanawake 100,000 wanaojifungua nchini Kenya, wanawake 488 huaga dunia.Mwanamke nchini Kenya nafasi 1 kati ya 38 ya kuaga wakati wa kujifungua ikilinganishwa na 1 kati ya 1600 ya mwanamke nchini Mauritius.

Wanawake pia ni asilimia 58 ya watu waliokomaa ambao wanaishi na virusi vya ukimwi.Hata hivyo, wanawake bado wana uwezo mkubwa wa kuishi miaka mingi zaidi ya wanaume.Mwanamke anatarajiwa kuishi miaka 55 ikilinganishwa na miaka 54 ya wanaume.

Kuhusu maswala ya ndoa,mwanamke wa kiwango cha wastani huolewa akiwa na miaka 21.4 huku mwanamme akioa na miaka 26.2.

Umri wa kuolewa wa msichana huongezeka kiwango cha elimu kinapoongezeka, Uchunguzi uliofanywa hivi karibuni unaonyesha kuwa wasichana ambao hawajaelimika huolewa wakiwa na miaka 17.5 huku wale ambao wamesoma hadi kiwango cha shule ya upili wanaoleka wakiwa na umri wa miaka 22.4.Hii ni karibu miaka mitano baadaye.

Wanawake katika kiwango cha chini kabisa kiuchumi, huolewa wakiwa na miaka 18.6 kwa kuwa ndoa ndiyo njia rahisi sana ya kuwatoa katika hali ya umaskini pale wanapoolewa kwa wanaume tajiri.Kwa upande mwingine, mwanamke katika kiwango cha juu cha kichumi huolewa akiwa na umri wa miaka 22.6 yaani miaka minne baada ya wale wa kiwango cha chini kiuchumi.

Kwa wastani, mwanamke chini Kenya ana watoto 5.0 akilinganishwa na wale wa kizazi cha mamake ambao ni 7.2 na wa kizazi cha nyanyake ambaao ni 7.5.

Wanawake na wanaume nchini Kenya wanatofautiana kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya watoto wanaopata. Wanaume wa mjini ambao wamehitimu elimu ya shule ya upili hupendelea kuwa na watoto 3.4 huku wale wa mashambani wakipendelea watoto 4.3.Kwa upande mwingine, wanawake ambao wana kisomo cha shule ya msingi wanaoishi mashambani hupendelea kupata watoto 4 ilhali wale wa mjini ambao wamehitimu kisomo cha shule ya upili hupendelea kupata watoto 3.
Kwa kuzingatia kipato, wanaume matajiri nchini Kenya hupata watoto 3.4 huku wale maskini wakipata watoto 6.
Kwa wanawake asilimia 20 ya wale matajiri hupata watoto 3 huku wale maskini wakipendelea kupata watoto 5.1
Nchi ya Kenya ina kiasi kikubwa cha wanawake wanaofanya kazi.Karibu 47 ya wafanyikazi ni wanawake. Hii ni idadi nzuri hasa kwa kuwa asilimia 50 ya watu nchini Kenya ni wanawake.Hata hivyo hali hii si ishara ya kupewa uwezo kwani wanawake wanahusishwa na kazi katika sekta zisizo rasmi,zisizokua na ambazo faida yake ni ya chini sana kama vile; ushonaji, kuuza mboga na kuchuuza.
(Dondoo kutoka gazeti la Nation tarehe 8 machi ,2012 ,UK iv)

MASWALI

(a) Wanawake na wanaume wanatofautiana kwa kiasi kikubwa.Kwa kurejereaa taarifa, thibitisha.(maneno 110-120)

(alama 9) (mtiririko 1)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

(b) Kwa ithibati mwafaka tofauti kati ya wanawake**.(maneno 50-60)**

(alama 4) (utiririko 1)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Bainisha mfumo wa sauti katika neno lifuatalo **(alama 2)**

Masalkheri

(b) Eleza matumizi manne ya kiimbo **(alama 2)**

(c) Tambulisha viambishi katika neno lifuatalo **(alama 4)**

Nilichokutenganishia

(d) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali **(alama 4)**

Mwanafunzi aliyepata gredi ya A hakuwa mvivu shuleni

(e) Fuata maagizo **(alama 2)**

(i) Mgonjwa amepewa dawa asubuhi(kauli ya kutendesheka mazoea)

(ii) Poa (Nafsi ya kwanza wingi, wakati ujao kauli ya kutendana.)

(f) Andika sentensi yakinishi kutokana na ifuatayo **(alama 2)**

Utawala mbaya wa Bokono haukuzuilika

(g) Bainisha mwingiliano wa maneno katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Walifunga ndoa juzi walakini ndoa yao ina walakini

(h) Tambua vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mwanafunzi aliyesoma kwa bidii alipita mtihani

(i) Tunga sentensi moja kubanisha matumizi ya vitate hivi **(alama 2)**

Ngoma

Goma

(j) Bainisha maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mwonyeshe atakavyosoma.....

(k) Tumia kitenzi kifuatacho kama kitenzi kisaidizi na kama kitenzi kishirikishi **(alama 2)**

Ndi-

(l) Mwalimu huyu atawatahini wanafunzi wote watakaofanya mtihani (anza wanafunzi wote) **(alama 2)**

(m) Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano **(alama 2)**

(i) ufisadi (unda kitenzi)

(ii) -pya (unda nomino)

(n) Tambua aina ya shamirisho katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mama alimpikia chakula

(o) Andika sentensi zifuatazo kwa udogo **(alama 2)**

(i) Chungu changu kimevunjika

(ii) Ng'ombe wangu ana ndama mkubwa

(p) Kwa kutolea mifano, elezea matumizi matatu ya mshazari (**alama 3)**

(q) Kwa kuzingatia nafsi,tambua na uonyeshe mofimo katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

(i) Sisi tunampenda yeye tu.

(r) Tambua kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo **(alama 1)**

Tulimkuta akiwa katika uchungu mwingi

4. ISIMU JAMII

Kuna madai kwamba lugha ya kiswahili ni zao la lugha za kibantu. Kwa mfano mitano thibitisha madai haya. **(alama 10)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 6 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili.
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
h) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

MASWALI

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

1.Lazima

a) ”Mwanangu nakuomba uzingatie uadilifu maishani uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu…”

i)Tambua kipera na utanzu wa tungo hili **(al. 2)**

ii) Kwa kutumia hoja **mbili** eleza muundo wa kipera hiki **(al. 2)**

iii) Fafanua sifa **nane** za kipera hiki **(al.8)**

b) Eleza vikwazo **vinane** vya ukuaji wa fasihi simulizi. **(al.8)**

SEHEMU B: RIWAYA

Assumpata k. matei: : chozi la Heri

Jibu swali la 2 au la 3

2.”Si kufua, si kupiga deki, si kupika…almuradi kila siku na adha”

a) a) Eleza muktadha wa kauli hii. **(ala.4)**

b) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. **(al.2)**

c) Kwa kutumia hoja **kumi na nne**, eleza maudhui yaliyodokezwa na dondoo hili. **(al.14)**

3.”Kila mara hujiuliza ikiwa watoto huwa na hadhi tofauti nje au ndani ya ndoa”

Amali inayotajwa imekumbwa na changamoto chungu nzima.Jadili kwa kurejelea riwaya nzima. **(al.20)**

SEHEMU C: TAMTHILIA

P. Kea : Kigogo

Jibu swali la 4 au la 5

4.”Acha porojo zako. Kigogo hachezewi;watafuta maangamizi!”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili **(al.4)**

b)Fafanua sifa za mzungumzaji **(al.6)**

c)Kwa kurejelea hoja **kumi**, thibitisha kwamba kucheza na kigogo anayerejewa ni sawa na kutafuta maangamizi **(al.10)**

5.”Tunahitaji kuandika historia yetu upya.”

a)Eleza sababu **kumi na mbili** kuonyesha kwa nini ilikuwa muhimu kuiandika historia ya sagamoyo upya **(al.12)**

b)Onyesha mikakati inayotumiwa kuiandika upya historia ya Jumuiya ya sagamoyo **(al.8)**

SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

LONGA
Longa longea afwaji, watabusarika
Longa uwape noleji, watanusurika
Longa nenea mabubu,sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno
Longa usidakihizwe,kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tenge si noma
Longa pasi wasiwasi,ongea kalima
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma
Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa
Longa liume wakora, kwani wezi miwa

Longa bangu na parara, hawakuitiwa
Longa bunge si kiwara, si medani tawa
Longa ni simba marara, wanaturaruwa.

Maswali

a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili **(al.1)**

b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi **(al.4)**

c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. **(al.4)**

d) Eleza aina **tatu** za urudiaji katika shairi **(al.3)**
Tambua na ueleze **toni** ya shairi **(al.2)**

e) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi. **(al.2)**
i. Afwaji
ii. Tenge

f) Eleza umbo la shairi hili. **(al.4)**

7.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Kila nikaapo husikia tama
Na kuwazia hali inayonizunguka

Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Hujiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu jinsia ya kike
Hukaa na kujidadisi
Hujidadisi kujua ni kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Wezangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuikosea utamaduni

Hukaa na kujiuliza
Iwapi raha yangu ulimwengu huu?
Iwapi jamaa nzimaa ya wanawake?

Maswali

a) Taja sifa **mbili** za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili **(al.2)**

b) Eleza dhamira ya mshairi **(al.2)**

c) Kwa kutoa mifano, eleza maana ya mistari mishata **(al.3)**

d) Bainisha tamathali **mbil**i za usemi zilizotumika katika shairi hili **(al.4)**

e) Eleza nafsineni katika shairi hiri **(al.2)**

f) Tambua **toni** ya shairi hili **(al.2)**

g) Taja maudhui **matatu** katika shairi hili **(al.3)**

h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi **(al.2)**

Madhila

Kudhalilishwa

SEHEMU E: HADITHI FUPI

A. Chokocho na D kayanda : Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine.

8.”…hamna mwendawazimu wala mahoka kati yetu, mimi nimepewa zawadi hizo”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(al.4)**

b) Eleza sifa nne za msemaji **(al.4)**

c) Hakiki nafasi ya maudhui ya busara kwa mujibu wa hadithi hii **(al.12)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 7 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA
INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
i) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI.

1. Wewe umemaliza chuo kikuu hivi majuzi. Huku ukiambatanisha wasifukazi, andika barua ya kuomba kazi katika kampuni ya maji ya Nzoia kama mhasibu.

2. Technolojia mpya ya habari na mawasiliano(TECHNOHAMA) imeleta manufaa mengi nchini.
Jadili.

3. Mchuma janga hula na wa kwao.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya :
…..kila aliyesikia habari hizi shuleni mwetu alifurahi na kushangilia kwa vifijo na nderemo kwani ushindi huo ulikuwa umengojewa kwa muda wa miaka mingi.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 7 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

SEHEMU YA A :UFAHAMU (Alama 15)

Soma kifungu hiki kasha ujibu maswali.

Binadamu heshi kuwa na falsafa zinazojiri akilini mwake. Amejichanjia kijisayari chake na kufikirika mfano wa Mirihi katika falaki yake ya maisha. Ni sayari ndogo ambayo imejitenga na sayari nyingine kama vile kausi.

Mirihi kuna viumbe mauluti vyenye mitindo ya kustaajabisha. Tofauti na Kausi ambayo ambako mabinti huwa na urembo wa kiasilia, wanamirihi ni "warembo" mithili ya walioanguliwa ja vifaranga. Viganja vyao na nyuso zao huwa zimekandwa kwa mafuta ya zebaki zikawa nyororo japo wengi huwa mithili ya suriama. Wasalaminiapo na Wanakausi mikwaruzo yao huwachipua ngozi kwa kazi ya sulubu waifanyayo shambani. Fauka ya uchotara huo, wamefungasha kiasi huku wamejisetiri kwa vijisuruali na vijisketi ambavyo vimewabana kana kwamba vimeundwa kwa vitambaa vya mikononi na kutafuta misaada kutoka kwa majirani kuvivua na kuvivaa

Wanakausi waliovalia nguo zinazowafika kwenye visigino, huchushwa mno na hivi vijiguo vinavyowasetiri hadi kwenye sisemi vilegesambwa, ukipenda magotini, bali kwenye mapaja. Ni kweli kwamba waso haya wana mji wao. Wanapondatia hasa kwenye hafla za maziko au arusi katika sayari ya Kausi Wanakausi hujibana pembeni kujionea malimweng ulimwenguni. Minong'onezo ndio itajaa hewani " ni yakini Pemba ndiko kwenye nguo na wenda uchi wapo"

Katika hafla hizo, wale mabinti wazuri wa Mirihi hubeba **vibogoshi** ambamo mara kwa mara hutoa vidubwasha vidogo vidogo na kuendelea kujipodoa huku shughuli zinapoendelea. Pengine huenda umesahau kuwa katika mipango na makadirio ya matumizi ya hafla hiyo marejeleo yanayokaririwa huwa
"…wajua watu wa Mirihi hawapendi….."

Mabinti wazuri wa Mirihi kila mmoja huwa amejibebea mwavuli na kujizuia mvua au jua huku amekumbatia maji ya chupa ya kutoka kwenye ya Mirihi.

Wanakausi walalahoi huwa wakikata kiu yao rahisi kutoka kwenye mapipa yaliyojazwa maji au kwenye mifereji waliyobahatika kuwekewa na wizara ya maji, kwa kutumia viganja vya mikono. Mabwana wa Mirihi hawana haja na miavuli, wao huwa watu wenye zao. Huvalia kofia nene zinazoonekana kama somberero. Watembeapo huning'iniza funguo za magari ya kifahari katika mkono wa kushoto na simu ya rununu katika mkono wa kulia

Hapa na pale watakuwa wakiwasiliana kwa simu zao na pia kupiga gumzo na maghulumu wa
Kausi ambao kwa kawaida watakuwa wakiwarai Wanamirihi,"**Utaniacha hivyo"**

Baada ya hafla, mlo ambao huwa Wanamirihi hupakukuliwa huku Mabwanamirihi wakidakia wasichelewe, mabintimirihi wakinyofoa kwa mikono au kung'ofoa kwa midomo yao myekundu na Wanakuasi wakichungulia kwa mbali wakisubiri nafasi yao itimie.

Ghafla mawingu yataanza kutanda upande wa mashariki na mambo sasa yatachukua mkondo mpya. Wanamirihi mchakamchaka huengaenga, mbio kwenye magari yao. Lakini

kuna wale ambao hawana magari ya kukimbilia. Kawaida yao huwaita Wanamirihi wenzao faraghani "Baba fulani umejaza?"

Wengine hubaki kusema, "Uenda basi letu likaniacha, tutaonana nikija wikendi."

Hali iwapo mwanana, Wanakausi watakuwa sasa ndio wakati wa kujitambulisha na wengine kuyajaza magari ya Wanamirihi ya kifahari kwa maembe, avokado, ndizi na makochokocho ya vitu vya shambani. Baada ya miezi kadha, Wanakausi wachache watawazuru Wanamirihi kuwapa shukurani katika kijisayari chao cha Mirihi.

Hapo sasa watavumbua jibu la kitendawili watakapokumbana na Bintimirihi amebeba kijikaratasi cha nailoni kimejazwa embe dondo moja, sukuma wiki, bila kusahau kisehemu cha nyama alichopimiwa cha shilingi kumi. Kwa kuwa atapata malazi kwake atamshauri, "…..pengine unionyeshe bucheri tununue nyama…tupitie dukani tununue……" hapo kwake Malaika atakuwa ameshuka kutoka Kausi hadi Mirihi.

Lakini wengine ni wale ambao pindi tu utakapowasalimia watakukwa na "zamu ya usiku siku hiyo." Wanaovalia somerero watamlaki Mwanakausi kwa mlahaka wa kifalme ili akastaajabie vitu kama **Majirafu,** mazulia, makochi, taja nitaje.

Yule wa awali atalala usiku huo usingizi mnono usio na bugudha na kwenye kochi huku akihimiria kurauka mapema asikutwe na waliolala nyuma ya pazia. Hisia za Mwanakausi zitamrudisha katika tamthilia ya Wole Soyinka "Masaibu ya ndugu Jero kuwa "vidole vyote havikuumbwa sawa." Mirihi ni sayari iliyosheheni watu na viatu, kumbe Kausi ni shamba la paukwa na pakawa la Edeni.

Tafakari haya.

Maswali

a) Andika anwani mwafaka ya taarifa hii **(Alama 2)**

b) Eleza tofauti kati ya wanawake wa Mirihi na wale wa Kausi. **(Alama 2)**

c) "Mabwana wa Mirihi ni watu wenye zao". Thibitisha. **(Alama 3)**

d) Ni dhahiri kuwa Mirihi ni sayari yenye watu na viatu. Nini maana ya viatu.

Je, kuna viatu hapa?

Thibitisha. **(Alama 3)**

e) Mwandishi anamaanisha nini anaposema "Utaniacha hivyo?" **(Alama 2)**

6. Eleza maana ya: **(Alama 2)**

i) Jirafu

ii) Vibogoshi

SEHEMU YA B:UFUPISHO **(Alama 15)**

Katiba mpya imeipa lugha ya Kiswahili hadhi nyingine kuifanya kuwa lugha rasmi kando na kuwa ni lugha ya taifa. Mabadilliko haya muhimu yana changamoto kadhaa:

Kwanza kabisa lugha ya Kiswahili sasa itashindania nafasi sawa na ile ya kiingereza katika shughuli za kikazi. Swala hapa linahusu majukumu ambayo lugha hizi zitatekeleza. Je, lugha hizi zitatumika mtawalia katika shughuli za kikazi au zitatengewa majukumu maalum?

Lugha ya kswahili itachukua nafasi ipi? Kiingereza kitaachiwa nani tukizingatia kuwa kwa muda mrefu lugha ya kiingereza ndio imekuwa lugha tawala katika mazingira haya? Je, wananchi wataweza kufanya maombi ya kazi kwa lugha ya Kiswahili kando na kuendesha mawasiliano ya kiofisi kwa lugha hii. Kwa kifupi ili kusitokee mgongano wa matumizi ya lugha hizi mbili ni muhimu sana kwa watungasera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili katiaka mazingira ya kikazi.

Changamoto jingine na muhimu ni kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya. Kwanza, wananchi wanafaa wafahamishwe kuhusu haki yao ya kutumia lugha hii katika mazingira ya kazi. Si ajabu kuwa wengi wao hawana habari kuhusu mabadiliko haya ya kisera. Watumishi wa umma nao wanastahili kupewa mafunzo maalum kuhusu mbinu za mawasiliano katika kiswahilli waendeshe shughuli zao vizuri.

Kwa upande mwingine, vyuo vikuu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zinastahili kutoa kkozi ya lazima katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga nazo ili kuwaandaa kwa mahitaji haya mapya ya kikatiba. Kadhalika, serikali inastahili kuwandaa wataalamu zaidi wa lugha ya Kiswahili ambao watahuusika katika kuwafunza wanaohusika na utekelazaji sera.

Kuna haja pia ya wataalamu wa lugha kuandika vitabu zaidi kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vitatoa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za mawasiliano. Shughuli hii iambatane na ile ya kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha zingine kwa ile ya Kiswahili.

Kwa muda mrefu sasa, kumekuwa na tatizo la mtazamo hasa miongoni mwa wananchi kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wananchi wamekuwa na sababu zao za kutoitumia lugha hii wakishikilia kuwa lugha yenyewe ni ngumu.

Aidha, wananchi wengi wamekuwa na uzoefu wa kuzungumza lugha ya kiingereza au lugha nyingine za kigeni huku wakitoa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili. Serikali inastahili kutafuta njia ya kuwahimiza wananchi wote kuionea fahari lugha ya kiswahiili, waipende na kuielewa vizuri.

Ni muhimu kufanywe kila juhudi kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia Kiswahili sanifu ili wasije wakakivuruga kwa kukiendeleza visivyo au kwa kukiharibu kwa kijilugha cha sheng au kw alugha za kienyeji.

Vile vile ni muhimu wananchi watambue kuwa nchi yetu ya Kenya ndiyo kitovu cha lugha hii na hivyo basi wafanye kila juhudi kuitumia ipasavyo ili tusionekane kuwa watumwa katika lugha yetu asili. Tunahitaji viongozi vielezo nchini ambao wanazungumza Kiswahili sanifu kwa madoido na ufasha sio tu katika ulingo wa kisiasa bali pia katika nyanja nyingine za maisha.

Kwa hivyo, viongozi wetu wajiepushe na matumizi ya Kiswahili chapwa ili wananchi wahimizike kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Ingekuwa hata bora ikiwa wangepewa kipaumbele katika kupokea mafunzo kabambe katika lugha hii. Pengine

tungejifunza mengi kutoka nchi jirani ya Tanzania ambayo kwa kiasi kikubwa ilifaulu kurasmisha Kiswahili na kuleta umoja wa kitaifa.

Maswali

a) Eleza changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili(Maneno 80) **(Alama8)**

Maandalizi

Jibu

(b) Fupisha aya ya mwisho (Maneno 25)

Maandalizi

Jibu

SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA **(Alama 40)**

a) Taja sauti mbili ambazo ni vipasuo vya mdomo **(Alama 2)**

b) Tunga sentensi ya neno moja yenye sehemu zifuatazo **(Alama 3)**

i) Ngeli

ii) Wakati

iii) Kirejeshi

iv) Mzizi

iv) Kauli

v) vKiishio

c) Taja ngeli za majina yafuatayo **(Alama 2)**

i) Uga

ii) Kiroboto

d) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatvyo: **(Alama 2)**

i) Kiwakilishi nafsi kiambata

ii) Kiwakilishi ngeli

e) Andika kwa kinyume **(Alama 1)**

Kijakazi aliangika vyombo vya tajiri wake.

f) Unda nomino dhahania kutokana na vitenzi hivi: **(Alama 2)**

i) Cheza ii) Pika

g) Tunga sentensi sahihi kukbainisha tofauti kati ya maneno haya: **(Alama 2)**

i) Jua ii) Juha

h) Andika katika ukubwa. **(Alama 1)**

Sungura ambaye alikatwa mkia aliingia nyumbani.

……

i) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii. **(Alama 2)**

Alipiga teke mpira ukaruka juu juu zaidi.

j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. **(Alama 4)**

Mto ule uliofurika jana umezoa taka nyingi.

k) Kanusha. **(Alama 1)**

Jembe hilo ndilo nitumialo kulima shamba langu.

l) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo: **(Alama 2)**

Mtoto mwenye bidii hufanya vyema.

m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano **(Al 2)**

i) Tua (Tendama)

ii) Fumba (Tendata)

n) Eleza matumizi mawili ya ritifaa na utolee mifano kwa kila moja. **(Al 2)**

o) Andika katika usemi wa taarifa. **(Alama 2)**

"Nitakuja kesho asubuhi. Inshallah!" Bakari alisema.

p) Eleza maana mbili inayotokana na sentensi hii. **(Alama2)**

Aliletewa ng'ombe na mtoto wake.

q) Yakinisha. **(Alama 2)**

Asiposhiba hatafunguliwa.

r) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vifuatavyo: **(Alama 2)**

i) 'a' unganifu

ii) Amba-rejeshi

s) Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu. **(Alama 3)**

Hapa ndipo alikofia.

t) Iweke sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu.

(Alama 1) Aliomba msamaha kwa kuchelewa.

SEHEMU YA D: ISIMU JAMII **(Alama 10)**

a) Eleza sababu nne zinazowafanya watu kubadili msimbo. **(Alama 4)**

b) Mazungumzo ya mahakamani husheheni sifa zipi? **(Alama 6)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 7 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: 2 ½

MAAGIZO

a) *Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima*

b) *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki*

c) *Usijibu maswali **MAWILI** kutoka sehemu moja.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
JUMLA	80	

SWALI LA LAZIMA

1.HADITHI FUPI ALAMA 20

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE :Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda

Mtihani wa Maisha

6. *"..Acha nijiondokee duniani niwaachie wafanisi wafanikie."*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **Alama 4**

b) Taja na ufafanue sifa tatu za msemaji. **Alama 6**

c) Eleza jinsi maisha ya msemaji yanavyoafiki anwani ya hadithi. **Alama 10**

2.RIWAYA CHOZI LA HERI : Assumpta Matei ALAMA 20

7. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri.

Alama 20

8. *"...liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **Alama 4**

b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili.**Alama 6**

c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo"**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. **Alama 10.**

3.TAMTHILIA KIGOGO : Pauline Kea ALAMA 20

9. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka." Jadili.

Alama 20

10. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo

i) Kinaya **Alama 6**

ii) Majazi **Alama 8**

iii) Jazanda **Alama 6**

4.FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

6. **a)** Eleza **aina** tano za wahusika wa fasihi simulizi. **Alama 10**

b) Eleza sifa za wahusika wa mighani. **Alama 10**

7. **a)** Eleza namna amabavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji.Toa hoja nne. **Alama 8**

b) Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. **Alama 4**

c) Taja viungo vinavyopambanua muundo wa nyimbo katika jamii **Alama 4**

d) Andika majukumu manne ya nyimbo katika jamii **Alama 4**

5.USHAIRI ALAMA 20

8. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia,namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,

Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

Maswali

(a) Shairi hili ni la kimapokeo. Toa sababu mbili **kuunga** kauli hii. **(Alama.2)**

(b) Taja **bahari kuu** ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. **Fafanua**. **(Alama.2)**

(c) Fafanua dhamira ya mshairi. **(Alama.2)**

(d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. **(Alama.2)**

(e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. **(Alama.2)**

(f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. **(Alama.4)**

(g) Mshairi anamaanisha nini anaposema _zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,‘ **(Alama.2)**

(h) Eleza toni ya shairi hili. **(Alama.2)**

(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao.

i) Nitatongoa

ii) Zitapusa. **(Alama.2)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 8 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Insha zote **sharti** ziandikwe kwa kijitabu cha majibu
h) Karatasi hii ina kurasa mbili zilizopigwa chapa.

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Wewe ni katibu wa kamati ya upatanisho nchini.
Andika kumbukumbu za mkutano uliopigia darubini mizozo ya kijamii.

2. "Simu za rununu zimeleta faida nyingi kuliko hasara".
Jadili.

3. Baa hukutia mtu wako.

4. Andika insha itakayoanzia kwa maneno haya:
Abiria walishauriwa kufunga mikanda ya usalama.
Utingo mmoja alikejeli, "Hili nalo litafika?"**…….**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 8 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswall yanayofuata

Ikolojia ni elimu ya kisayansi inayohusu uhusiano wa kimazingira kati ya vitu vyenye uhai (mimea na wanyama) na visivyokuwa na uhai (hali ya hewa udongo Elimu ya ikolojia ipo katika mfumo wa elimu ya mazingingira). Mfumo huu umegawanyika katika sehemu mbili: mfumo wa mazingira ya nchi kavu, na mfumo wa mazingira ya majini (bahari, maziwa, mito na madimbwi).

Viumbe wamejirekebisha kulingana na mazingira yao. Kwa mfano samaki wana matamvua yenye uwezo na kusharabu hewa ndani ya maji Ngo'mbe wana mapafu ya kuvuta hewa katika nchi kavu. Sehemu za mvua ya kawaida zina majani manene ili yaweze kuhifadhi maji nyakati za shida. Mimea, wanyama, udongo na viathiri vingine vya hali ya hewa vinahusiana sana kimazingira. Mimea huota kutegemea hali ya nchi, umbo au sura ya ardhi na aina ya udongo

Hali ya nchi ni wastani wa hali ya jotoridi, wastani wa mvua, unyevunyevu hewani, upepo, msukumo na mwanga kwa muda wa miaka thelathini. Dunia imegawanyika katika kanda mbalimbali. Kila kanda ina mimea na wanyama wa aina yake kutegemea hali ya nchi. Ukanda wa istiwai una joto, mvua na unyenyevu mwingi. Miti ya ukanda huu hufanya misitu minene, yenye miti mirefu. Miti hii ni mirefu kwa sababu ya msongamano unaofanya miti igombanie mwanga wa jua kwa kurefuka. Katika misitu hii, ipo mimea ya kangaga inayotambaa na kukwea miti mingine. Katika ukanda wa Savanna, hali ya joto na mvua si kubwa kama katika ukanda Wa istiwai. Kwa sababu hii, sehemu nyingi ni vichaka na nyika zenye uwezo wa kuota nyasi zisizohitaji mvua.

Upepo una faida na hasara katika mazingira. Upepo husaidia kusukuma mawingu yaletayo mvua. Upepo unapozidi hudhuru mimea na wanyama kwa sababu hukausha mali ardhini, huvunja na kuharibu mimea, huleta vifo kwa wanyama na pengine kuharibu mazingira ya watu. Mimea katika mazingira hutegemea sana nuru ya jua ili kutengeneza chakula chake Kiasi cha mwanga upatikanao mahali fulani huathiri mimea na wanyama wapatikanao katika mazingira yale.

Maswali

a) Pendekeza anwani kwa taarifa uliyosoma **(alama 1)**

b) Eleza maana ya ikolojia **(alama 2)**

c) Kwa nini wanyama huwa na sifa mbalimbali za kimaumbile **(alama 2)**

d) Ni kwa vipi ukanda wa istiwai unatofautiana na ukanda wa Savanna? **(al 3)**

e) Ni kwa namna gani upepo unaweza kuwa na athari mbaya kwa mazingira? **(alama 4)**

f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu **(ala 3)**

i) Matamvua

ii) Kusharabu hewa

iii) Istiwai

2. MUHTASARI

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Vijana wengi, wake kwa waume, walikuwa ndio tu wakamilishe shughuli ya kusajiliwa chuoni. Walikuwa bado nadhari zao zimetekwa na ugeni, hawajapata starehe akilini mwao wala kujisikia wamekaribia kama kwao nyumbani.Kwa hakika mazingira yale mapya yalikuwa yanawapa kiwewe kidogo au tuseme hata woga kiasi. Kusema kweli, kwa wakati ule walikuwa hawajui ni maisha ya namna gani yanayo wasubiri mahali pale. Hawakuweza kukadiria kwa uyakinifu wowote iwapo makaazi yao pale ya miaka minne mizima kuanzia wakati ule, yangekuwa na utulivu na raha au pengine yangeondokea kuwa ya roho juu juu na matatizo chungu nzima. Walisubiri.

Walimsubiri mkuu wa Chuo aingie wasikize atakalosema waweze kubashiri vyema mkondo wa maisha yao utakavyokuwa. Lakini jinsi walivyosubiri Mkuu wa Chuo aingie ukumbini ndivyo wayo wayo lao lilivyozidi kuwacheza shere. Waliwaza: ugeni jamani kweli ni taabu. Mawazo mengi yaliwapitia bongoni mwao. Wakawa kimya ukumbi mzima, kama kwamba wamekuja mazishini badala ya kuja kusoma.
Waliwaza na kuwazua. Waliona au pengine walidhani kuwa hapa kila kitu ni tofauti.

Wanafunzi hawa waliona tofauti nyingi kati ya mambo pale chuoni na yale waliyokuwa wamezoea. Kwa mfano, mwalimu Mkuu hapa hakuitwa ‘headmaster” kama kule katika shule za msingi na vile vile shule za upili, bali aliitwa ‘vice-chancellor”. Nyumba za kulala hazikuitwa ‘dormitory’ au ‘mabweni’ .kama walivyozoea, bali ziliitwa ‘halls’ kwa sababu sio kumbi za aina yoyote ile bali ni nyumba hasa, zenye vyumba vya kulala, kama nyumba nyingine zozote zile. Shule yenyewe haikuitwa shule au skuli, au hata chuo kikuu kama walivyozoea kuiita walipokuwa shule zao za upili huko, bali hapa wenyewe wenyeji waliita kwa majina mengine kabisa! Mara “University”, mara Zutafindaki, mara Ndaki kwa ufupi, mara Jamahiriya na kadhalika na kadhalika! Waliwaza: kweli mahali hapa panaweza kumkanganya mtu! Kwa kweli kabisa panaweza kumzubaisha mtu hadi kufikia kiwango cha kuonekana kama zuzu! Hata hivyo hawakuvunjika moyo, bali walipiga moyo konde wakanena kimoyomoyo: potelea mbali Ukiyavulia nguo, yaoge! Walikuwa wamo katika hali hii ya kurandaranda katika

ulimwengu wa mawazo pale katika ulimwengu wao mpya, ulimwengu mwingine kabisa usiofanana hata chembe na ule waliouzoea, Mkuu wa Chuo alipoingia.

Kuingia Mkuu wa Chuo, wote walisimama kwa pamoja na kwa mjiko, wamekauka kama askari katika gwaride. kuona hivyo, Mkuu wa Chuo akawaashiria wakae tu, bila kujisumbua. Kicheko kikawatoka bila kukosa adabu na heshima, kisha wakakaa kwa makini. Ndio mwanzo wakajisikia wamepoa. Kuona kuwa sasa wametulia na wamestarehe, Mkuu wa chuo akaanza kwa kuwaamkua, kisha akawajulisha kwa wakuu wa vitivo mbali mbali na idara mbali mbali waliokuwa wamekaa pale jukwaani alipo yeye upande huu na huu.
Kufikia hapo, alaka ikawa imeungwa baina ya wenyeji na wageni wao. Kila mtu akaona mambo yamtesibu tena, huo bila shaka ni mwanzo mwema, na kama ilivyosemwa na wenye busara, siku njema huonekana asubuhi. Hii, kwa wote ndiyo asubuhi: na si asubuhi tu, bali ni asubuhi njema, si haba.

Maswali

a) Ukirejelea aya ya kwanza na ya pili, eleza ni kwa nini wanafunzi walikuwa na wasiwasi. **(Maneno 45 - 50) (alama 6)**

Majaribio

Jibu

b) Ni mambo gani mageni ambayo wanafunzi walikumbana nayo, (Maneno 20 - 25) **(alama 3)**

Majaribio

Jibu

(c) Bila kupoteza maana, fupisha aya tatu za mwisho kwa kutumia maneno yako mwenyewe.

(Tumia maneno 40 - 45) **(alama 6)**

Majaribio

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) **(i)** Eleza tofauti za kimatamshi kati ya sauti zifuatazo. **(alama 2)**

/P/

/b/

(ii) Onyesha sehemu zinapotamkiwa sauti zifuatazo. **(alama 2)**

/dh/

/ch/

(b) Tumia neno 'safi' katika sentensi kama: **(alama 2)**

(i) Nomino

(ii) Kivumishi

(c) Andika udogo wa sentensi ifuatayo katika wingi. **(alama 2)**

Sahani hiyo imechafuliwa na mkono wake.

(d) Taja matumizi **mawili** ya kila moja ya viakifishi vifuatavyo.

(i) Parandesi

(ii) Ritifaa

(e) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo.

(alama 2) **Mwanafunzi** aliyejeruhiwa uwanja amevuja **damu.**

(f) Ainisha sehemu zote za: **(alama 3)**

Alimgombeza

(g) Tambua aina ya vishazi vilivyo katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Mwanafunzi aliyesoma amefuzu mtihani.

(h) Onyesha virai vilivyo katika sentensi hii. **(alama 2)**

Yule mwanabiashara amepata hasara kubwa.

(i) Andika kunyume cha: **(alama 2)**

Baba alimbariki mwanawe mtiifu.

(j) Kanusha sentensi hii. **(alama 2)**

Susan alifanya kazi kwa bidii na kufanikiwa maishani.

(k) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. **(alama 4)**

Baba, mama na mwanawe ni watundu lakini watashtakiwa kortini.

(l) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania. **(alama 2)**

(m) Andika katika usemi wa taarifa. **(alama 4)**

(i) "Njooni hapa!" baba akaamuru.

(ii) "Twende kwetu leo jioni". Msichana alimwambia mpenzi wake.

(n) Eleza maana mbili zilizo katika sentensi hii. **(alama 2)**

Baba mzazi amefika.

(o) Tambua na ueleze aina ya vitenzi katika sentenzi ifuatayo. **(alama 3)**

Huyu ndiye mwalimu aliyekuwa akisomesha.

(p) Maneno haya yako katika ngeli gani? **(alama 2)**

(i) Karatasi

(ii) Nyasi

(q) Tunga sentensi ukitumia kitenzi **la** katika kauli ya kutendwa. **(alama 2)**

(r) Weka shadda katika **neno** lifuatalo. **(alama 1)**

Nne

4. ISIMU JAMII

Tom: Vipi Tracey? Naona leo unalinga sana.

Umenivaria miwani, mbona hivi? Is it because you are very smart today?

Tracey: Niko poa! Hata hivyo naona una yako mengine wewe! Siringi! Nikobusy tu sana.

Plus company yako inatisha, hujui siku hizi nimechill.Tena umenubore.

Tom: Kumbe wewe ni……

(a) Taja sajili inayojitokeza katika dondoo hii. **(alama 1)**

(b) Taja mifano inayojitokeza katika dondoo ya

(i) Kubadili msimbo **(alama 1)**

(ii) Kuchanganya msimbo. **(alama 1)**

(c) Ni kwa nini wazungumzaji hubadili na kuchanganya msimbo. **(alama 2)**

(d) Ni mzungumzaji yupi ana lafudhi? Ni nini maana ya lafudhi? **(alama 3)**

(e) Taja sababu mbili za kuwa na lafudhi. **(alama 2)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 8 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako,shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A: USHAIRI

LAZIMA

1. ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Tunda ni kuliangua, chungwa liloninginia,
Tunda pia kuchumia, mbuga sima yowelea,
Jinginelo lipo?

Tunda kivuno shambani, lima kisha palilia,
Tunda vinono nyumbani, kwa jasho shughulikia
Jinginelo lipo?

Tunda tokeo la kazi, na ujira jipatia,
Tunda matokeo wazi, jitihada jifanyia,
Jinginelo lipo?

Tunda pia ni kizazi, wana hao niliozaa,
Tunda tama ya ulezi, wana wataponifaa,
Jinginelo lipo?

Tunda letu la uhuru, minyororo jikongoa,
Tunda sote kuwa huru, na mazao furahia,
Jinginelo lipo?

Tunda ni wetu uchumi, na chumo kujichumia,
Tunda mwenzangu huchumi, ukaweza kwendelea
Jinginelo lipo?

Tunda bora utu mwema, yako roho kuilisha,
Tunda la roho nasema, mja kumkamilisha,
Jinginelo lipo?

Maswali

(a) Shairi hili lina bahari kadha zitaje na ueleze. **(alama 4)**

(b) Eleza vina na mizani ya ubeti wa sita na saba. **(alama 4)**

(c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika shairi hili. **(alama 2)**

(e) Taja maana ya 'tunda' kama ilivyotumika katika shairi. **(alama 3)**

(f) Eleza maana ya maneno haya kama ilivyotumika katika shairi. **(alama 3)**

(i) Kuliangua

(ii) Palilia

(iii) Kujichumia.

SEHEMU YA B: FASIHI SIMULIZI

2. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Sungura alivyokwepa kuliwa na samba

Wanyama wa pori waliamua siku moja kumtuma mnyama mmoja kila siku alikoishi simba kama chakula. Siku moja ilikuwa zamu ya sungura kwenda huko. Sungura alikuwa mjanja sana. Alipanga mpango mzuri wa kumwangamiza simba.

Alienda alikoishi simba muda mrefu baada ya muda wa chakula wa simba. Alimkuta simba akiwa na hasira kubwa sana.

``Kwa nini umechelewa jinsi hii?`` aliuliza kwa hasira.

'Bwana wee,`` alisema sungura kwa sauti ya upole.

``Nilichelewa kwa sababu simba mwingine alinikimbiza. Nilitaabika sana kabla ya kupata upenyu wa kutoroka.``

``Simba mwingine? Je, katika pori hili?`` aliuliza samba.

``Ndiyo bwana mkubwa. Najua anakoishi. Tuandamane nikakuonyeshe,`` alisema sungura.

Simba alijitayarisha kuandamana na sungura. Sungura aliongoza njia hadi walipofika mahali palipokuwa na kisima kikubwa. Sungura alimgeukia na kusema, ``Anaishi hapa. Tafadhali njoo umuone!``

Simba alisogea ulipokuwa ukingo wa kile kisima. Aliyatupa macho huko na kukiona kivuli chake. Alidhani kuwa huyo alikuwa simba mwingine. Kwa hasira kubwa alifungua kinywa na kunguruma. Alimwona huyo simba mwingine akikenulia meno. Simba hakuweza kusubiri, alijitosa kisimani apambane na simba huyo. Huo ulikuwa mwisho wake. Sungura aliondoka akicheka akifurahi kuwa sasa wanyama hawataliwa tena na simba.

Maswali

a) i) Andika aina ya hadithi hii **(Alama 2)**

ii) Taja sifa tatu za kutambulisha aina hii ya hadithi **(Alama 3)**

iii) Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi kwa jamii **(Alama 3)**

b) Kwa kutoa mifano taja aina mbili ya fomyula ya: **(Alama 4)**

i) Kuanza hadithi

ii) Kumalizia hadithi

c) Eleza sifa nne za mtambaji bora katika fasihi simulizi **(Alama 4)**

d) Tofautisha kati ya vipera viwili vya fasihi simulizi.

i) Mighani na maghani **(Alama 2)**

ii) Lakabu na misimu **(Alama 2)**

SEHEMU YA C:

RIWAYA: CHOZI LA HERI:ASSUMPTA K.MATEI

3. Maovu yametamalaki katika jamii ya Riwaya ya Chozi la Heri, tetea kauli hii kwa kutolea hoja kumi **(alama 20)**

4. Auntie Sauna alishikwa na polisi "

a. Liweke dondoo hili katika muktadha wake **(alama 4)**

b. Huku ukitoa mifano, fafanua sifa tatu za msemaji **(alama 6)**

c. Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hii **(alama 2)**

d. Ni kwa nini Auntie Sauna alishikwa na polisi? Elezea kikamilifu **(alama 8)**

SEHEMU YA D:

TAMTHILIA : KIGOGO: PAULINE KEA

5. Ami? Tangu lini ukawa ami yangu? **(ALAMA 20)**

a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama2)**

b) Taja mbinu iliyotumika katika dondoo hili. **(alama2)**

c) Eleza sifa za Msemaji **(alama8)**

d) Bainisha maudhui ya nafasi ya mwanamke ukizingatia mhusika huyu. **(alama8)**

6. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika Tamthlia hii. **(alama 20)**

a) Kinaya

b) Majazi

SEHEMU YA E

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE

HADITHI FUPI: ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA SHIBE INATUMALIZA

7. "Ndugu yangu kula kunatumaliza"

"Kunatumaliza au tunakumaliza"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Fafanua maana ya kitamthali katika kauli 'kula tunakumaliza' **(alam 10)**

(c) Kwa mujibu wa hadithi hii, ni kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? **(alama 6)**

AU

8. (a) "Mame Bakari"

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka. **(alama 10)**

"Masharti ya Kisasa"

"…mapenzi ni mateso,ni utumwa, ni ukandamizaji , ni ushabiki usio na maana."

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi**.** **(alama 10)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 9 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Kumekuwa na kongamano shuleni mwako kuhusu umuhimu wa katiba mpya nchini Kenya.

Wewe ukiwa katibu, andika kumbukumbu za kongamano hilo.

2. Eleza madhara ya uharibifu wa mazingira.

3. Vita vya panzi neema ya kunguru.

4. Malizia kwa ".....hapo ndipo nilitambua kuwa ukabila ni ugonjwa mbaya usiostahili kuweko katika taifa lolote lile.

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 9 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kufikia miongo michache iliyopita, ujumbe ulisafirishwa kwa njia zilizochukua muda mrefu sana kufika. Kwa mfano, mtu alipotaka kupiga simu katika nchi jirani barani Afrika, ilimbidi kupitia kwa opareta katika nchi za Ulaya ndipo aunganishwe. Kupigia simu kutoka Gambia kwenda Senegal ilibidi kutumia opareta wa kule London na wa Paris, Ufaransa, na wa Senegal.

Leo hii kuna njia nyingi za mawasiliano zilizo bora, za kutegemewa na zinazofikisha ujumbe kwa kasi sana. Ujumbe ambao ungechukua muda mrefu kuufikisha, sasa unapelekwa kwa sekunde moja. Miongoni mwa njia hizi ni mdahilishi, simu tamba na tuama, faksi, satelaiti, mitandao ya wavuti, n.k. Hamna eneo sasa hivi hata liwe mbali vipi lisilofikika na aina hizi za mawasiliano.

Maendeleo haya ya mawasiliano yamechangia pakubwa sana kuufanya ulimwengu kuwa kijiji kimoja. Sasa kuna uhusiano wa karibu sana miongoni mwa mataifa duniani katika nyanja zote za maisha. Hali hii ndiyo inayoitwa utandawazi au utandaridhi. Utandawazi umeleta mabadiliko mengi maishani.

Mojawapo ni utoaji na uzalishaji wa mali. Mabadiliko ya mawasiliano yameruhusu mashirika ya kimataifa kusambaza utoaji na uzalishaji wa bidhaa zao katika maeneo mbalimbali duniani. Hali hii imepunguza gharama za usafirishaji sana. Bidhaa inayoundwa na kiwanda chenye hakimiliki kilichoko kule New York masafa ya mbali, inaweza kuzalishwa na kiwanda kilicho hapa Nairobi. Bila shaka umesikia kuhusu madawa ya kurefusha maisha ya wahasiriwa wa UKIMWI ambayo yanazalishwa na baadhi ya viwanda vya kutengeneza madawa humu nchini. Kiwanda chenye hakimiliki kipo jijini London.

Viwanda ambavyo vilikuwa katika mataifa tajiri kama vile Uingereza, Ufaransa, Marekani,Ujerumani na Japani sasa vimeweza kutandaza vitandabui vyake kote duniani. Utandazaji huu hufanywa kwa njia kadhaa. Kwanza, viwanda hivi huvinunua viwanda vilivyoko katika mataifa yanayostawi. Vinaweza kuingia katika **ubia** na viwanda vya mataifa wanakotaka kuhamia, Viwanda hivi vya mataifa yanayoendelea hupatana kuwa watasimamia utoaji na uzalishaji wa bidhaa fulani na kukubaliana namna yn kugawa mapato.

Utandawazi katika sekta ya uzalishaji na utoaji bidhaa umeleta manufaa kadhaa katika nchi zinazoendelea,- .Mojawapo ya haya ni kupatikana kwa nafasi za kazi. Pili, bidhaa za nchi zinazoendelea ambazo hazingeshindana na zile za mataifa yaliyoendelea sasa zimepata nafasi ya kushindana. Halikadhalika, wateja wana nafasi ya kupata bidhaa watakayo bila kuvunjwa moyo. Iwapo bidhaa anayohitaji mteja haipatikani katika nchi, inaweza kuagizwa moja kwa moja kutoka kwa kiwanda kingine chenye uhusiano nacho. Uagizaji hauchukui muda

kutokana na hali ya mawasiliano inayoweza kutegemewa na inayofikisha ujumbe bila kupoteza wakati. Fauka ya haya, wateja hupata uwanja mpana wa kuchagua wanachokihitaji.

Utandawazi umehimiza kustawi kwa mazingira ya mashindano katika utoaji na uzalishaji mali viwandani. Sasa hivi hamna nehi yenye uwezo wa kufungia bidhaa za nehi nyingine katika nilpaka yake. Kufanya hivi ni kujitia kitanzi kiuchumi. Lazima nchi zifungue masoko yao. Navyo viwanda vya kimataifa huweza kuwania masoko haya. Matokeo yake ni wateja kufaidika kwa kupata uwanja mpana wa bidhaa za kuchagua. Wateja pia hupata bidhaa za hali ya juu na kwa bei isiyo ghali kutokana na mashindano haya. **Mashindano ya kimataifa ni kama ya paka na panya na kiwanda kisichojifunga nira** vizuri, huwa kinajihatarisha. Kinaweza kujipata kimetupwa nje ya soko na kuangamia.

Manufaa rnengine ya utandawazi ni kuwa watu sasa hivi wanaweza kuwasiliana kwa urahisi na wepesi. Kwa kutumia simu, au mdahilishi, mtu anaweza kuwasiliana na mwenzake popote alipo licha ya masafa. Zaidi ya haya, utandawazi umewawezesha watu kutoka asili mbalimbali kuingiliana na **kutangamana**, Utangamano huu umeweza kuleta umoja baina ya watu kwa kutohoa hisia za ubaguzi.

Hata hivyo utandawazi umetokeza kuwa na madhara. Kwanza uchumi wa nchi nyingi umeibukia kutawaliwa na matukio ambayo hayazihusu nchi hizo moja kwa moja. Uvamizi wa kijambazi wa Septemba 11, 2000 kule Marekani uliathiri uchumi wa nchi nyingi sana. Matukio ya vita katika Mashariki ya Kati nayo yamechangia kuzorotesha uchumi wa nchi nyingi hasa zile maskini ambazo zinategemea mafuta kutoka huko ilhali vita hivyo haviwahusu sikio wala ndewe.

Athari kubwa ya utandawazi yaonekana katika sekta ya kijamii. Tamaduni nyingi za jamii katika nchi maskini zinaendelea kuvurugwa na maadili kuporomoka kutokana na ustawi wa kimawasiliano. Vijana wanaiga kutoka mataifa ya kimagharibi bila kuchuja. Si ajabu kuwa vijana wetu wanavaa mavazi **yasiyositiri** uchi wao vizuri na yasiyostahiki kwa jina la ustaarabu.
Wavulana nao huzidisha kwa **kutoga** masikio na kusuka nywele usiweze kuwatofautisha na dada zao.

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alm1)**

2. Kwa nini hapo awali watu walipitia opareta walipokuwa wakipiga simu? **(alm1)**

3. Eleza ubora wa mbinu za mawasiliano ya kisasa zikilinganishwa na za zamani **(alm2)**

4. Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa mawasiliano **(alm3)**

(i) Yamechangia pakubwa sana kufanya ulimwengu kuwa kijiji kimoja?

(ii) Viwanda vilivyokuwa katika mataifa tajiri. . . sasa vinaweza kutandaza vitandabui vyake kote duniani

(iii) Mtu anaweza kuwasiliana na mwenzake. . . licha ya masafa.

5. Eleza jinsi ambavyo utandawazi katika sekta ya uzalishaji na utoaji umeziathiri nchi zilizostawi. **(alm2)**

6. Taja mikakati inayotumiwa na mataifa yaliyostawi kutandaza vitandabui vyao **(alm2)**

7. Fafanua maana ya mafungu haya kama yalivyotumika katika kifungu. **(alm4)**

(i) Utandaradhi

(ii) Kutangamana

(iii) Miongo.

(iv) Yasiyositiri

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu.

Magonja hayo yamewahangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha saria nyakati fulani za histori ya binadamu. Magonjwa haya yaliwauwa maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno “UKIMWI” lilitolewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno “UKIMWI” humanisha Ukosefu wa kinga mwilini, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonjwa

wa UKIMWI umepewa majina kama vile 'umeme' na pie 'ugonjwa wa vijana'. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini. Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethibitishwa kwamba takriban watu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutkana na kuambukiza virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima yakuishi, badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonjwa hu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kupitia juhudi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

(a) Kwa kutumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha aya nne za mwanzo (maneno 60 – 70) **(alm11)**

Nakala Chafu

Nakala Safi

(b) Eleza mambo yanayoleta matumaini kwa wagonjwa wa UKIMWI kulingana na aya mbili za mwisho (maneno 20 – 30) **(am4)**

Nakala Chafu

Nakala Safi

3. Matumizi ya Lugha

(a) Ni fonimu gani haifai kuwa miongoni mwa zingine? Toa sababu. **(alm2)**

Ng', g, t, k

(b) Fafanua matumizi ya kiambishi 'ku' katika sentensi ifuatayo. **(alm2)**

Hakukuletea.

(c) Tunga sentensi ukitumia nomino inayotokana na kitenzi. **(alm2)**

Abudu

(d) Kanusha ukitumia 'O' rejeshi. **(alm2)**

Migomba ambayo hupaliliwa vizuri hunawiri sana.

(e) Andika katika usemi wa taarifa. **(alm2)**

Je, tutazuru Mombasa lini? Aboi aliwauliza wanafunzi.

(f) Ainisha vielezi namna katika sentensi ifuatayo. **(alm3)**

Walikimbia haraka sana wakilia kwikwikwi.

(g) Andika katika ukubwa wingi. **(alm3)**

Mwanamume huyu ana ng'mbe mmoja na mbwa.

(h) Tumia vinyume vya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi ifuatayo.

(alm2)

(i) Tumia kihusishi 'katika' kwenye sentensi kuonyesha:

(i) Mahali

(ii) Wakati

(j) Changanua kwa njia matawi.

Mapambo yaliyonunuliwa na Bakari ni ya Pakistan. **(alm4)**

(k) Kando na kuonyesha king'ong'o hafa toa mfano mwingine wa matumizi ya ritifaa. **(alm1)**

(l) Andika sentensi hii katika kauli ya kutendeana.

Farida alimlea mtoto wa Farizana naye Farizana akamlea mtoto wa Farida.

(m) Yakinisha. **(alm2)**

Msiposoma kwa bidii, hamtafanya vizuri katika mtihani.

(n) Tunga sentensi tatu ukitumia neno harka kama;

(i) Nomino

(ii) Kielezi

(iii) Kitenzi

(o) Toa maana mbili zinazodhihirika katika sentensi hii. **(alm2)**

Yeye ndiye mwalimu pekee wa Kiswahili.

(p) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia maagizo ya mabanoni. **(alm2)**

Wanafunzi wote walipita mtihani isipokuwa mmoja. (Anza Hakuna ..... ila....)

(q) Tumia kitenzi ‘vuka’ kutunga sentensi katika hali ya kuamrisha. **(alm1)**

(r) Andika sentensi katika hali isyodhihirika. **(alm1)** Aliimba akioga.

(s) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo. **(alm2)**

(iv) Sabuni

(v) Zabuni

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Mhusika X: Hebu sema majina yako kamili?

Y: Mussa bin Maksuudi.

X: Ulisema unataka kukata rufani?

Y: Ikiwezekana.

X: Usitie shaka umepata presidential amnesty.

Y: Alhamdulillah. Nitaenda Mskitini Ijuma kuabudi na kumshukuru Mungu.

Maswali

(a) **(i)** Taja muktadha wa mazungumzo haya **(alm2)**

(ii) Toa sababu ya kuthibitisha jibu la (a) hapo juu.

(b) Tambua wahusika **X:.....**

Y:.....

(c) Taja na kutoa mifano ya sifa zozote tatu za lugha inayotumika katika mazungumzo haya. **(alm6)**

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 9 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili.
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
h) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU A. RIWAYA YA CHOZI LA HERI

1. " …na ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde ,vitisho na matusi ?"

i. Eleza mukatadha wa dondoo hili**.** **(Alama 4)**

ii. Taja na ueleze umuhimu wa tamathali ya usemi uliyotumika dondooni. **(Alama4)**

iii. Mabadiliko ni aushi. Jadili kwa kurejelea riwaya nzima ya Chozi la Heri. **(al 12)**

SEHEMU B. TAMTHILIA YA KIGOGO. (Alama 20)

2. " Kama mmeletwa hapa na umbeya,naona mmekosa njia"

(a) Weka maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b) Jadili jinsi ambavyo msemaji na wenzake wenye hulka sawia walivyopotea njia.

(Alama 5)

(c) Eleza dhima sawia za wasemewa. **(Alama 5)**

(d) Eleza vizingiti vyovyote sita wanavyopitia wanaharakati tamthiliani. **(Alama 6)**

3. Jadili mbinu zifuatazo kama zilvyotumika katika tamthilia ya kigogo. **(alama 20)**

a. Uwili

b. Jazanda

c. Majazi

d. Tashtiti

SEHEMU C. TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO

4. " Nafurahi maana najua hakuna mtoto mwengine wa mtu atakayekatishwa tamaa na …"

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. **(Alama 4)**

b. Onesha kinaya kinavyojitokeza katika dondoo**.** **(Alama2)**

c. Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi ya mwalimu mstaafu. Thibitisha. **(alama 14)**

5. Vijana wamekumbwa na changamoto nyingi katika jamii. Tathmini kauli hii ukirejelea hadithi zifuatazo.

Tulipokutana tena.

Mtihani wa maisha

Shogake dada ana ndevu

Ndoa ya mashaka

SEHEMU D. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

6. Dunia hadaa,ulimwengu shujaa.Mnachohitaji mlipofikia, ni ujasiri wa simba kuyakabili maisha.Adabu na bidii yenu leo, ni miche itakayozaa matunda, matunda matamu ya maisha mema kesho.Sitaki muziandame nyendo potovu . Mtakuwa mnajiponza wenyewe ; na hilo litakuwa sawa na kuutumbukiza mustakabali wenu kwenye shimo lenye kina kirefu na giza totoro.Jueni ujana ni moshi na ukienda haurudi.

(a)

i. Tambua kipera hiki na utoe ithibati**.** **(Alama 2)**

ii. Ni sifa zipi za kipera hiki zilizojitokeza hapom juu. Eleza kikamilifu **(alama 5)**

(b) Misimu hutumia mbinu anuwai katika uundaji wake. Taja tano na utolee mifano mwafaka.. **(Alama 5)**

(c) Eleza mbinu ambazo ungetumia kufanikisha kipera hiki. (Alama 8)

7.

a) Eleza maana ya miviga**.** **(Alama 2)**

b) Taja sifa tano za miviga**.** **(Alama 5)**

c) Pendekeza njia tatu za kuhifadhi kipera cha miviga**.** **(alam 3)**

d) Eleza udhaifu wa mbinu zifuatazoza ukusanyaji data ya fasihi simulizi.

(i) Hojaji **(alama3)**

(ii) Kushiriki **(alama 3)**

e) Fafanua matatizo yanayomkabili mtafiti wa fasihi simulizi nyanjani. **(alama 4)**

SEHEMU E. USHAIRI

Swali 8.

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno

Basi pasiwe na choyo, na usonono

Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno

Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano

Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano

Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano

Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono vyanda vitano

Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano

Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano

Naazibe masikiyo, asisikie maneno

Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, juu wetu Muungano

Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano

Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno

Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano

Daima tuwe ni ngao, palipo msagurano

MASWALI

(i) Huku ukitoa mifano thibitisha kuwa shairi hili ni sala. **(alama 4)**

(ii) Liweke shairi hili katika bahari mbili ukitumia: **(alama 2)**

Idadi ya

(i) Mishororo
(ii) Vina

(iii) Onyesha muundo wa shairi hili. **(alama 5)**

(iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 3)**

(v)ukitoa mifano eleza umuhimu wa idhini zifuatazo kama zilivyotunika katika shairi**.** **(Alama 4)**

a) Inkisari
b) Mazda
c) Kuboronga sarufi
d) Tabdila

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)

(i) Usonono –
(ii) Msagurano –

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 10 PAPER 1

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

Muda: Saa 1 ¾

Maagizo

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **Lazima**
d) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
e) Kila insha isipungue maneno **400.**
f) Kila insha ina alama 20
g) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili

Kwa matumizi ya matahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
2	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Wewe kama mtaalamu wa mazingira umeshuhudia ukataji wa miti nchini bila kupanda mingine.Andika barua kwa mhariri ukilalamika tendo hili kwa kueleza madhara yake.

2. Fafanua vikwazo vinavyokumba elimu ya bure nchini. **(alama 20)**

3. Upweke ni uvundo. **(alama 20)**

4. Andika insha itakayoanzia na:

Woga ulitoka mafichoni mwake na kutuvamia kama jeshi la usabi…..

FOR MARKING SCHEMES CALL 0705525657/ 0707550000

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 10 PAPER 2

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

MUDA: Saa 2 ½

Maagizo

1 *Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
2 *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
3 *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali*

Kwa matumizi ya mtahiniwa pekee.

Swali	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

SEHEMU A : UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Utalii ni sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Mamilioni ya watalii huzuru nchi yetu kila mwaka ili kujionea madhari ya kuvuta pamoja na mbuga za wanyama zenye ufahari wa kimataifa. Wanyama wa mbugani wanaopatikana ni kama vile ndovu, kifaru, twiga, simba, chui na ndege kama kongoni, flamigo,tai,mbuni na kadhalika. Wanyama hawa na ndege huwavutia sana watalii kiasi cha kuwapiga picha kuzihifadhi ili wafikapo makwao waweze kuwaonyesha jamaa zao ambao nao huingiwa na shauku ya kataka kuvinjari katika nchi yetu ya Kenya.
Watalii wanapofika nchini huimarisha pato kubwa kutokana na fedha nyingi za kigeni wanazoipatia nchi hii kama ushuru. Wanapotembelea mbuga za wanyama pia hutoa ada Fulani ya fedha ambazo husaidia kuongeza pato letu Ia kiuchumi, Katika hoteli au mikahawa wakulima humu nchini hupata fursa ya kuyauza mazao yao kama vile mboga, matunda, mayai, nyama na kaclhalika na kupata riziki zao. Vijana wengi ambao wamekuwa wakirandaranda mitaaani hupata nafasi za ajira za kazi mbalimbali kama vile unajimu, upishi, ulinzi, ukalimani na kadhalika. Wengine huajiriwa kama madereva au waelekezi wa watalil hawa.

Watalii pia huiinarisha uhusiano mwema baina ya nchini yetu na nchi tofauti tofauti wanazotoka. Uhusiano huo hudumisha amani na utangamano nchini. Watalii hawawezi kuzuru nchi ambayo inakoosa amani.

Hata hiyo, kama waswahili walivyosema hakuna mchele ukosao ndume. Shughuli za utalii katika nchi, nyetu zimetuletea madhara si haba. Baadhi ya watalii huja nchini na kuleta mila na desturi zao ambazo si nzuri sana. Kwa mfano watalii mara nyingi hawaoni haya wanapotembea wakiwa nusu uchi huku.

Wakishikana mikono na kupigana pambaja hadharani. Haya ni mambo ya kustajaabisha hasa sisi Waafrika. Baadhi ya vijana nao hujiingiza katika uhusiano wa kimahaba na watatli hao wa kike na hata wa kiume. Huu ni utovu wa nidhamu kwa vijana wetu.

Licha ya watalii kutuletea fedha nyingi za kigeni tunaona kuwa faidha tunayopata kutoka kwao Si nyingi sana. Kwa mfano, watalii husafiri kwa ndege zinazotoka mashirika yao. Hata mahoteli vanayosafiria watalii pia ni ya makampuni ya kutoka kwao kama vile ‘pollmans’, ‘ust’ ‘francorcissaco’ ..’utc’na kadhalika.

Ingekuwa bora kama watalii wote wanaotaka kuingia nchini wawekewe masharti ya kusafiri kwa shirika Ia ndege Ia ‘Kenya Airways’. Wafikapo hapa wajipumzishe na kustarahe katika mahoteli yanayomilikiwa na Wakenya. Kisha wasafirishwe kwa

kutumia usafiri wa umma kama vile magari ya matatu'. Hapo ndipo tutakapoweza kupata faida kemkem kutokana na utalii.

Tukitazama kwa makini tutaona kuwa faida za utalii ni chache kuliko hasara zake. Hata hivyo, utalii Si lazima uwe wa wageni peke yake hata Wakenya wanaweza kuwa utalii.

MaswaIi

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka **(al.2)**

b) Watalii wanaozuru nchi yetu huvutiwa na nini? **(al.2)**

c) Eleza faida za kiuchumi zinazopatkana kutokana na shughuli za utalii **(al2)**

d) Mwandishi alimaanisha nini aliposema kuwa kuna mchele ukosao ndume. **(al.2)**

e) Eleza hasara zinazopatikana kutokana na utalii. **(al.2)**

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. **(al.2)**

i) Mandari:

ii) Usguru:

iii)

Ukalimani:

iv) Kupigana pamoja :-

v) Utovu:

SEHEMU B : UFUPISHO **(ALAMA 15)**

Soma makala yatuatayo kisha ujibu maswali

Ushirikiano wa kiuchumi hauwezi kufanyika shaghabaghala. Lazima yawepo mapatano Fulani Kiuchumi. Leo tunaishi katika kipindi ambapo mazungumuzo kuhusu utandawazi yameshika nguvu sana

Msingi mmojawapo Wa utandawazi ni kuondolewa kwa vikwazo vya kibiashara katika mataifa mbalimbali ili kuimarishwa ulimwengu mzima lakini uondoaji huu wa lazima pia uwe na msingi Fulani ghafla wa bidhaa rahisi ambazo zinatishia viwanda na biashara changa. Kwa njia hii biashara change katika mataifa yenye uchumi mjini Arusha,Tanzania. Bunge ni chombo muhimu katika kujadili na kupitisha makubaliano yanayoathiri utendakazi au jinsi shughuli mbalimbali zinavyoendeshwa.

Bunge la Afrika Mashariki linaweza kupitisha sheria ambazo zitaudhibiti utendakazi na shughuli za wenyeji wa Afrika Mashariki. Pia linawea kupitisha sheria zinazodhibiti biashara na maingiliiano ya wenyeji wa nchi zetu hizi. Zipo juhudi za kuhakikisha kuwa pana mahakama inayoshughulikia masuala ya jumuiya hii mpya. Chombo hiki kitakuwa msingi katka kulikabili suala la usalama katika rnataifa yetu haya. Kama tujuavyo, hamna taifa linaloweza kuendelea vizuri ikiwa usalarna wake hauna uhakika. Kila mfanyibiashara na mwekezaji anapenda kufanya biashra kuwekeza katika mazingira ma zuri.

Maswali

a) Mbunge Ia Afrika Mashariki na mahakama yana umuhimu gani katika nchi za jumuiya ya Afrika Mashirika.

Matayarisho

Jibu

b) Fupisha aya mbili za kwanza baina ya maneno 60— 70. (al. 7) **(2 mtiririko)**

Matayarisho

Jibu

MATUMIZI YA LUGHA : (ALAMA 40)

a) Taja ala mbili tuli za kutamkia **(alam 2)**

b) **Eleza maaana mbili za sentensi ifuatayo.** **(alama 2)**

Farida ni mkulima wa pekee kijijini mwetu

c) **Nomino zifuatazo ni za aina gani ?** **(al. 2)**

a) **Umati wa watu :**

b) **Wino** :

d) **Andika upya kwa kusingatia hali katika mabano.** **(al.4)**

a) Mtoto alikunywa maji ya matunda (Kutendeshwa)

b) Waumini walitoa fungu la kumi.(kufanyiza)

e) **Nyambua vitenzi hivi katika hali ya kutendesha.** **(ala. 2)**

a) **La**

b) **Vuka**

f) Jaza nafasi wazi kwa kiambishi 'ndi' pamoja na kiashiria cha ngeli kifaacho. (ala.3)

i) Sisi ……wakubwa wao

ii) Selina ……kiranja wa darasa hili iii) Nyinyi …… Walezi wa watoto hawa.

g) Onyesha mizizi katika maneno yafuatayo. (ala. 2)

a) Wataruka

b) Mtoto

c) Wanamcha

h) Ainisha vishazi katika tungo hizi. (ala. 3)

a) Mwalimu anafunza vizuri . **(ala 1)**

b) Kiti kilichovunjika kilitengenezwa na seremala. **(ala. 2)**

9. **Taja vokali inayoona na maelezo yafuatayo. (ala. 2)**

a) Vokali ya mbele, nchini

b) Vokali ya nyuma, juu

10. Eleza matumizi ya kiambishi 'ka' katika sentensi ifuatayo: (ala.2)

11. **Unda nomino kutokana na vintenzi hivi. (ala. 2)**

i) Onea

ii) Umia

12. Andika kwa wingi . (ala. 2)

Kuwepo kwa mshairi wake kulimfurahisha waziri

13. Andika kwa usemi wa taarifa. **(ala. 2)**

« Lo ! kumbe wazuri hawajazaliwa, » Omari alisema baada ya kumwona kisura huyo.

14. **Onyesha aina za shamirisho katika ifuatayo . (ala. 3)**

Mama alimakatia mgeni muwa kwa panga.

15. Pigia mstari kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo.

(ala.1) Bakari alikuwa miongoni mwa wanahewa.

16. Kwa kutumia jedwali, changanua sentensi ifuatayo : (ala. 5)

Rooney aliyechaguliwa alicheza mpira kistadi.

ISIMU JAMII

a) Eleza umuhimu wa sajili. **(ala. 5)**

b) Toa sababu tano zinazowafanya watu kuchanganya ndimi wanapozungumza.

(ala.5)

CROSSCOUNTRY MOCKS

KISWAHILI

TRIAL 10 PAPER 3

NAME…… INDEX NO……..…

SCHOOL…….. SIGN……..….

DATE……..

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A:

1. LAZIMA. FASIHI SIMULIZI

a) Eleza vitambulisho vya mtambaji bora wa hadithi. **(alama 4)**

b) Fanani huihusisha hadhira kwa njia gani? **(alama 4)**

c) Eleza mbinu mlumbi anazoweza kutumia ili afanikishe uwasilishaji wa ulumbi

(alama 12)

SEHEMU YA B: JIBU SWALI LA 2 AU LA 3 .

TAMTHLIA : KIGOGO

2. "Wamenimaliza… wamenigeuka."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.

b) Eleza namna msemaji alivyomalizwa na kugeukwa. **(alama4)**

c) Eleza umuhimu wa mnenaji wa dondoo hili**.** **(alama 4)**

d) Eleza jinsi wahusika wengine walivyomalizwa katika tamthilia**.** **(alama 8)**

3. Utawala wa jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka."Jadili usemi huu.**(alama 20)**

SEHEMU YA C.

4. **Ushairi: Jibu swali la 4 au la 5**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Nyoosha mkono, uviringe ngumi, unyanyuwe kwa hasira.
Nyoosha mkono, sema hunitumi, ila haki ujira.
Nyoosha mkono, alama ya kukataa.
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, na macho makali, uwaonyeshe kukerwa

Nyoosha mkono , wataka halali , kwamba hutaki kuporwa
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu.

Nyoosha mkono, umekula njama, uyakatae madhila
Nyoosha mkono, nyanyua kwa hima, watambue hukulala
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu.

Nyoosha mkono, jiunge umoja, na wateswaji wenzako
Nyoosha mkono, mwonyeshe miuja, yaondoke masumbuko
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu.

Nyoosha mkono, ivume sauti, inayojaa kitisho
Nyoosha mkono, mumejizatiti kwa mengi maamrisho
Nyoosha mkono,alama ya kukataa
Alama ya nguvu.

Nyoosha mkono, mumeshikamana, huo ukuta wa chuma
Nyoosha mkono, kitisho hakuna , wao watarudi nyuma
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu.

Maswali

a) Bainisha bahari tatu zinazojitokeza katika shairi. **(alama 3)**

b) Andika ujumbe mkuu unaojitokeza katika shairi hili**.** **(alama 4)**

c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

d) Onyesha tamathali mbili za lugha zilizotumiwa. **(alama 2)**

e) Bainisha kwa njia tatu ni vipi mtunzi amefanikiwa kutumia uhuru wa kishairi **.(al 3)**

f) Tambua toni ya shairi hili **(alama 1)**

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

i) Madhila

ii) Jizatiti

AU

5. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

MWANA

1. Kwani mamangu, u ng'ombe, au punda wadobi?
Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

MAMA
2. Nong'ona mwana, nong'ona, nikaumiza umiyo
Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
Kwani kelele kunena, huyataki maishiyo?
Hilo nakwambia

MWANA
3. Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo
Nikabeba idhilali, ikautweza na moyo
Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo
Hebu niambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Nambie ipi sababu, ya pweke, kwenda kondeni
Nini ya, matulubu, kulima hadi jioni?
Na jembe ukidhurubu, ukilitua guguni
Yu wapi wako, muhibu, Baba kwani simuoni?
Hebu niambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mtaaani
Hajali hakuthamini, wala haoni huzuni
Mwisho haya ni nini , ewe mama wa imani?
Hebu niambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na kule kondeni kwako, ukatekuni kwa shoka
Ufunge mzio wako, utosini kujitwika
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
Ukichelewa vituko, baba anakutandika Hebu niambie

Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Chakula kilicho ndani,ni jasho lako hakika
Kisha mbioni, wapita kupokapoka
Urudi nje mekoni, uanze kushughulika
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka Hebu niambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

MAMA
Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
Ninaanza kujipinda, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia.

Maswali

a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili**.** **(alama 2)**

b) Shairi hili ni la aina gani? Toa ithibati. **(alama 2)**

c) Yataje mambo yoyote matano anayoyalalamikia mwana. **(alama 5)**

d) Eleza kanuni zilizotumika kusarifu ubeti watatu. **(alama 5)**

e) Andika ubeti wa nane kwa lugha tutumbi **(alama 4)**

f) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika shairi hili

i) Jaza **(alama 1)**

ii) Muhibu **(alama1)**

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI:

Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.

Jibu swali la 6 au la 7.

6. a) Jadili matatizo yanayowakumba wakazi wa madongoporomoka katika Tumbo Lisiloshiba**.** **(alama 10)**

b) Ubadhirifu wa mali ya umma umetamalaki katika hadithi ya Shibe Itatumaliza. Jadili kwa kutoa mifanomwafaka. **(alama 10)**

AU

7. "Aliyeumwa na nyoka akiona ung'ong'o hushtuka ."

a) Weka dondoo hil katika muktadha wake**.** **(alama 4)**

b) Eleza namna mzungumziwa alivyoumwa na nyoka. **(alama 6)**

c) Eleza vile mzungumziwa anaendeleza maudhui ya ushauri na ukosefu wa utu. **(alama 10)**

8. CHOZI LA HERI

" Dada Umu, Di, ni mimi, Ni ndugu yenu. Ni hai . Auntie Sauna alishikwa na polisi."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Fafanua sifa tatu za msemaji **(alama 6)**

c) Taja tamathali moja iliyotumika katika dondoo. **(alama 2)**

d) Kwa nini Auntie Sauna alishikwa na polisi? Eleza kikamilifu. **(alama 8)**

THE END

THIS IS 1st SERIES OF KCSE CROSSCOUNTRY KISWAHILI MOCKS EXAMS TRIALS

FOR MARKING SCHEMES/ANSWERS

CONTACT THE FOLLOWING OFFICIAL CONTACTS FOR MORE LEARNING RESOURCES.

0707550000 / 0705525657

(mwalimupublishers@gmail.com)

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

CALL/TEXT 0705525657 / 0707550000

CALL/TEXT/WHATSAPP

0707550000 / 0705525657

mwalimupublishers@gmail.com

THIS IS A PRODUCT OF MWALIMU PUBLISHERS

POWERED BY MR ISABOKE

WERE PROUD OF YOU!

CONTACT MWALIMU PUBLISHERS FOR SERIES 2 QUESTIONS

SUCCESS

KILA LA HERI